
SPORTPESA APP
CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA





**Shamsa** Ford omba Mungu wanaume wasikupe majaribu

UKURASA 20

# MAISHA

Agosti 22, 2021 Nipashe · Baba, Mama na Mwana · *Jumapili*



Ukurasa 15

MAISHA NI NYUMBA
Hizi ndizo mbinu za kufanya jiko lako ling'ae wakati wote



Hivi ndivyo Lusekelo Martin Kilimba na Esta walivyoanza maisha yao ya ndoa takatifu

Iliyofungwa tarehe 12/6/2021 Kanisa la Morovian Mbalizi na kufuatiwa na sherehe iliyofanyika katika ukumbi wa Tughimbe Hoteli, Mbalizi Mbeya

HARUSI

Ukurasa 12

Vyakula hivi vinaimarisha mwili



Ukurasa 14

Ukurasa 13

SKAFU ... ESHA



UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Agosti 22, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0580680

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz · www.facebook.com/nipashetz · www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Samia awashusha pumzi wapinzani

• **Aagiza** marekebisho sheria uchaguzi, kuondoa vifungu vilivyosababisha wagombea kuenguliwa... *Endelea uk. 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea Ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2020, kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: NEC**

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**MJANE ALIVYOGOMBEWA KURITHIWA MIAKA MITANO**

MJANE Rose Bayo, mkazi wa Kijiji cha Endaswold wilayani Hanan'g mkoani...


## ACT Wazalendo yajitosa sakata kodi ya majengo kupitia LUKU

UKURASA 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store




Silaa



Gwajima

# Gwajima, Silaa matatani madai kulichafua Bunge

UKURASA 4

**MICHEZO** KIVULI CHA MIQUISSONE CHATESA UK.24 · **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Samia awashusha pumzi wapinzani

Na Romana Mallya

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema hawana budi kuziangalia sheria ili zisitumike kuwanyima watu haki wakati wa Uchaguzi Mkuu.

Amesema wa masuala ya kiufundi, mathalani pale mtu anapokosea kuandika herufi za jina lake au za chama chake, yasitumike kumnyima haki ya kushiriki uchaguzi.

Mkuu wa nchi aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam alipopokea taarifa ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka jana iliyowasilishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Kauli hiyo iliyoonekana 'kushusha pumzi upinzani', ilipokewa kwa kushangiliwa na baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani waliohudhuria hafla hiyo, hata Rais akakiri kushangilia kwao kulionyesha imewagusa.

"Nadhani mipango ingewekwa vizuri zaidi, nilijua vyama vya siasa mtashangilia zaidi hili, kwa sababu tuliwashughulikia kweli uchaguzi uliopita, kila mlipokosea tuliwaweka pini na mkatupa fursa za kupita bila kupingwa.

"Suala hili kwa sasa litaangaliwa vizuri lakini muwe makini vinginevyo... ushauri uliotolewa hapa utatiliwa maanani na yale yote yatakayokwenda kuchambuliwa baada ya ripoti hii, serikali itayachukua na kuyafanyia kazi ipasavyo.

"Shukrani zangu ziende kwa vyama vya siasa na wagombea wote walioshiriki kwenye Uchaguzi Mkuu. Kwa namna ya pekee nakipongeza chama changu, Chama Cha Mapinduzi kwa kupata ushindi mkubwa na kwa kuwa mimi ni mwenyekiti, nawashukuru wanachama, wapenzi, mashabiki na wananchi waliopiga kura," alisema.

Rais Samia alisema katika uchaguzi huo, yapo matatizo yaliyojitokeza na hiyo ndiyo moja ya sababu ya kuandaliwa kwa ripoti hiyo na kuwekwa hadharani ili kutoa fursa kwa wadau wa uchaguzi na wananchi kuichambua na kutoa mapendekezo yao.

Alisema Mwenyekiti wa NEC ametaja baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na wadau mbalimbali yenye lengo la kuboresha uchaguzi ujao.

"Ametoa mapendekezo ya uwezekano wa kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa Sura 292.

"Mapendekezo mengine ya Uchaguzi Mkuu na wa serikali za mitaa kusimamiwa na mamlaka moja na mengine ni kuhusu uwezekano wa kuwa na watendaji wa tume hadi kwenye ngazi ya halmashauri.

"Mengine ni serikali kutoa fedha kwa ajili ya asasi za kiraia zinazotoa elimu ya mpigakura, mapendekezo yote haya ni ya kimsingi, mathalani suala la kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi kama alivyozisema zile sura ni la msingi pia," alisema.

Rais Samia alisema kitu cha umuhimu ni wadau kujadili kwa kina kwa sababu kila jambo linaloanzishwa lina msingi wake.

## • NEC yataka sheria mpya ya uchaguzi ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi



Mabalozi walioapishwa na Rais Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani), wakila kiapo cha uadilifu kwa viongozi wa umma, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. PICHA: IKULU

Aliwaomba wadau wakakae na kuyaangalia mapendekezo yaliyotolewa na wayapeleke serikalini waone namna watakavyoyafanyia kazi.

"Changamoto ninayoiona ni pale tulipotakiwa serikali kuwa na wasimamizi wa kudumu wa uchaguzi mpaka ngazi ya halmashauri ambapo itasababisha kuwa na bajeti kubwa sana.

"Pendekezo la kusaidia asasi za kiraia nalo litabebesha mzigo mkubwa wa fedha serikalini, lakini yote yanazungumzika na yanaweza yakafanyiwa kazi," alisema.

Rais Samia pia alizungumzia ushiriki kwenye uchaguzi na kubainisha kuwa licha ya kuwapo kwa idadi kubwa ya wanawake kuliko wanaume, idadi ya waliojitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi ilikuwa ndogo.

"Kati ya wagombea 30 wa nafasi ya urais na wagombea wenza, wanawake walikuwa ni saba tu, kwenye ubunge kati ya wagombea 1,257 wanawake walikuwa 293, kwenye udiwani wanawake walikuwa 668 kati ya 9,231.

Rais Samia alizihimiza asasi za kiraia kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha wanawake kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kwenye uchaguzi.

Pia alisema vyama vya siasa navyo viwaamini kwa sababu nchi haiwezi kupata maendeleo endapo zaidi ya nusu ya wananchi wake ambao ni wanawake watabaki nyuma.

Akizungumzia matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Rais alisema dunia ipo kwenye mapinduzi ya viwanda na shughuli nyingi za uchaguzi duniani zinafanyika kwa TEHAMA, hivyo wajipange kwenye mwelekeo huo kwa maeneo yanayoweza kutumia.

"Tukiweza kutumia TEHAMA, tutashirikisha wananchi wengi zaidi kwa sababu wengine wanashindwa kupiga kura kwa sababu wanakuwa kwenye majukumu mbalimbali, tukiwawekea mfumo mzuri watapiga," alisema.

Pia aliipongeza tume kwa kukamilisha ripoti hiyo huku akiyataja malengo makuu mawili ambayo ni kuashiria kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu na kuweka wazi taarifa yake ili wadau waichambue na kuainisha matatizo yaliyojitokeza na kutoa mapendekezo kwa ajili ya uchaguzi ujao.

"Ninawapongeza viongozi wa vyama vya siasa mlioshiriki tukio hili, uwapo wenu sio tu unadhihirisha umuhimu wa tukio hili bali kudhihirisha siasa siyo uhasama.

"Ni kweli uchaguzi uliopita CCM ilipata ushindi mkubwa lakini halijawazuia kuhudhuria tukio hili, mmeonyesha ukomavu wenu wa kisiasa," alisifu.

Rais Samia alisema ili uchaguzi ukidhi malengo, ni lazima usimamiwe vizuri, kinyume chake unaweza ukawa chanzo cha fujo na vurugu kama ambavyo imekuwa ikishuhudiwa katika baadhi ya nchi.

Aliipongeza tume kwa kusimamia uchaguzi wa mwaka jana na kueleza kuwa hakuna shaka kwa yeyote aliyeshiriki au kushuhudia, ulifanyika vizuri na kwa kiwango cha juu.

"Mwenyekiti wa tume ametaja mambo yaliyofanyika kufanikisha Uchaguzi Mkuu kuwa ni vifaa vilikuwapo vya kutosha na vilifika kwenye maeneo husika kwa wakati.

"Kwa mara ya kwanza zilikuwapo karatasi maalum za kupiga kura kwa wenzetu wasioona kupiga kura bila usaidizi," alisema.

Pia aliwapongeza Watanzania kwa kugharamia uchaguzi huo ambapo kiasi cha Sh. bilioni 416.8 kilitumia (Sh. bilioni 154.3 kwa ajili ya kuliboresha daftari la mpigakura na Sh. bilioni 262.5 kwa ajili ya mchakato wa uchaguzi wenyewe).

"Hili ni jambo kubwa ndugu zangu na ulimwengu haukufikiria tungeweza lakini tumeweza, ni matumaini yangu kwamba kama ilivyosemwa mwisho wa uchaguzi mmoja ni maandalizi ya uchaguzi mwingine, na huko mbele tutaweza kujisaidia wenyewe, tuanze kujipanga sasa," alisema.

Rais Samia aliwashukuru viongozi wa dini kwa kuliombea taifa katika kipindi chote cha uchaguzi na vyombo vya ulinzi wa usalama kwa kusimama imara na kuufanikisha kumalizika kwa amani na vyombo vya habari kwa kutoa taarifa na kuhamasisha mchakato huo.

Alizipongeza asasi za kiraia kwa kutoa elimu ya mpigakura na Watanzania kwa uchaguzi uliofanyika.

### KUTOKA NEC

Akisoma taarifa hiyo, Mwenyekiti wa NEC, Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Semistocles Kaijage, alisema imegawanyika katika sura 12 zinazoonyesha utekelezaji wa hatua mbalimbali za mchakato kuanzia maandalizi ya bajeti ambayo ilifanyika kwa awamu mbili.

Alisema awamu ya kwanza ilikuwa ni ya uboreshaji wa daftari la kudumu la mpigakura ambapo Sh. bilioni 154.3 zilitumika kugharamia ununuzi wa vifaa vya uboreshaji, uchapishaji wa nyaraka mbalimbali, mafunzo kwa watendaji ya uboreshaji na utoaji wa elimu ya mpigakura.

Jaji Kaijage alisema bajeti ya awamu ya pili ilikuwa ni ya Uchaguzi Mkuu ambapo Sh. bilioni 262.5 zilitumika kugharamia ununuzi wa vifaa na huduma kama karatasi za kura, vituturi, masanduku ya kura, uchapishaji wa nyaraka mbalimbali, mafunzo kwa watendaji wa uchaguzi na elimu ya mpigakura.

Alisema fedha hizo zililipwa kupitia mfuko mkuu wa Hazina na kwa mara ya kwanza serikali iligharamia shughuli hizo zote kwa asilimia 100 bila kutegemea msaada.

Alisema tume ilizipokea na kuzifanyia uamuzi jumla ya rufani 165 za wagombea ubunge na rufaa 67 kati ya 98 sawa na asilimia 68 zilizoomba wagombea kurejeshwa katika orodha ya wagombea zilikubaliwa na rufani 31 sawa na asilimia 22 zilikataliwa.

Alisema kati ya rufani 67 zilizoomba kuondolewa kwa wagombea walioteuliwa kwenye majimbo ni rufani tatu tu sawa na asilimia 4.5 zilikubaliwa hivyo rufani 64 sawa na asilimia 95.5 zilikataliwa na wagombea waliendelea kugombea ubunge kwenye maeneo yao.

"Kwenye udiwani wasimamizi wa uchaguzi walipokea na kufanyia uamuzi jumla ya mapingamizi 1,228, tume ilipokea, ilisikiliza na kuzitolea uamuzi rufani 451, rufani 235 kati ya rufani 389 sawa na asilimia 60.41 ambazo wagombea waliomba warejeshwe kwenye orodha ya wagombea zilikubaliwa.

"Rufani 154 kati 389 sawa asilimia 39.59 ambazo wagombea waliomba warejeshwe kwenye orodha ya wagombea zilikataliwa," alikumbusha.

Alisema rufani zote 62 ambazo warufani waliomba wagombea waondolewe kwenye orodha zilikataliwa.

Alisema matatizo yaliyojitokeza kwenye eneo hilo ni malalamiko kutoka baadhi ya vyama vya siasa na wagombea kuwa hawakupata matokeo ya rufani zao ambazo kimsingi hazikuwahi kupokewa wala kusajiliwa na tume.

Alisema baada ya uchaguzi, ambao hawakuridhika walifungua kesi na nne zilipinga matokeo ya ubunge na kesi 11 za udiwani.

Mwenyekiti huyo alibainisha vikwazo vilivyojitokeza ni pamoja na mlipuko wa corona wakati wa uborosheaji wa awamu ya pili ya daftari la mpigakura mpaka upigaji kura, kuharibika kwa miundombinu kuathiri usambazaji wa vifaa kwenye baadhi ya maeneo na idadi kubwa wananchi waliopoteza kadi za mpigakura au kuharibika.

Mengine ni mwitikio mdogo wa wapigakura katika baadhi ya maeneo, taasisi zilizopewa kibali cha kutoa elimu ya mpigakura kushindwa kufanya hiyo na madai ya baadhi ya mawakala wa vyama vya siasa katika baadhi ya maeneo kuzuiwa kuingia kwenye vituo vya kupigia kura.

Alisema wadau wa uchaguzi wa tume wanapendekeza kutungwa kwa sheria ya uchaguzi ambayo itawezesha tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi, kuwe na watendaji wa tume hadi ngazi ya halmashauri na mamlaka ziangalie kuunganisha sheria ya taifa ya uchaguzi na sheria ya serikali za mitaa ili kurahisisha utekelezaji.

"Usimamizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa usimamiwe na mamlaka moja, sheria za uchaguzi zitafsiriwe kwa Kiswahili, serikali iangalie namna ya kuziwezesha asasi za kiraia na taasisi zinazotoa elimu ya mpigakura, wagombea ubunge na madiwani wanaopita bila kupingwa wapigiwe kura," alisema.

# Waziri aona fursa utaalamu wa lugha

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, ametoa wito kwa Watanzania wenye utaalamu wa ukalimani na wanaojua lugha za kimataifa waende Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kupata mafunzo na baadaye kusajiliwa ili watumike kitaifa na kimataifa.

Aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akizindua vifaa vya ukalimani vilivyonunuliwa na serikali kwa gharama ya Sh. milioni 187.5 ili kuwezesha kuwafundisha wakalimani.

Waziri Bashungwa aliliagiza BAKITA kutumia vifaa hivyo kwa ajili ya kuwaandaa wakalimani wa kutosha ili nchi iwe na uwezo wa kuwapeleka katika mikutano kulingana na mahitaji ya kimataifa.

"Lazima tuwe na wakalimani wa kutosha ili watumike ndani na nje ya nchi pindi kunapokuwa na uhitaji huo, BAKITA tumieni vifaa hivi kuwaandaa wakalimani ili nchi iwe na uwezo wa kuwapeleka katika mikutano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa na tuondokane na bahati mbaya ya mkalimani wakati wa kufasili kutojiandaa vizuri," alisema.

Waziri Bashungwa alitoa wito kwa Watanzania ambao wanajua lugha za kimataifa zikiwamo Kiingereza, Kireno, Kichina, Kifaransa, Kijerumani na Kiarabu waende kwenye baraza hilo kupata mafunzo ya kisasa ya kutumia vifaa hivyo vilivyonunuliwa na serikali.

"Ninawaagiza mtengeneze kanzidata ya wakalimani wetu kimtandao ili nchi mbalimbali waweze kupata fursa ya kuingia huko na kuchagua wanaowahitaji kwa ajili ya kwenda kutoa huduma hii kimataifa, tumieni teknolojia ya kisasa, mkitaka utaalamu zaidi muwasiliane na wizara," alisema.

Waziri huyo alisema lugha ya Kiswahili kwa sasa inatumika katika mikutano mbalimbali ya kimataifa kama vile Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Bunge la Afrika na Umoja wa Afrika.

Alisema ili Kiswahili kiendelee kutumika katika mikutano mingine zaidi, lazima kuwe na wakalimani wa kutosha watakaokuwa wanatoa huduma ya ukalimani kwa Kiswahili kutoka lugha mbalimbali za kimataifa.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Pauline Gekul, alisema haipendezi kwa nchi mpaka sasa kanuni zinazotumika zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

"Haipendezi kanuni na sheria mbalimbali za wizara wakati tupo na BAKITA bado zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

"Ninadhani hili BAKITA mngelichukua mkaanza na kanuni za wizara yetu kisha tukashirikiana na wizara nyingine ili kuziweka katika lugha ya Kiswahili, ziwe rafiki na Watanzania," alisema.

# Mjane alivyogombewa kurithiwa miaka mitano

**Na Jaliwason Jasson,** HANAN'G

MJANE Rose Bayo, mkazi wa Kijiji cha Endaswold wilayani Hanan'g mkoani Manyara, anadaiwa kuishi kwa mateso na wanawe kwa miaka mitano baada ya kufungiwa na shemeji zake barabara ya kupita kutokana na kugoma kurithiwa.

Licha ya kumzuia kupita katika barabara hiyo, haikutosha shemeji zake hao waliamua kujenga kaburi feki ili kuwazuia kupita na kwenda kwenye shughuli zao ikiwamo kupitisha mazao.

Akizungumzia kisa hicho baada ya kutatua mgogoro huo, Mkuu wa Wilaya ya Hanan'g, Janeth Mayanja, alisema juzi kuwa:

"Baada ya kupata malalamiko ya mjane huyo, nilitembelea na kukagua kiwanja namba 1106, Kitalu 'A' kinachomilikiwa na mjane Rose Bayo ambaye mume wake alifariki dunia mwaka 2016.

"Baada ya mume wake kufariki dunia, shemeji zake walitaka wamrithi na baada ya kukataa ndipo mgogoro ulianza. Baada ya kubaini unyanyasaji huo, nilikwenda pale na kuainisha barabara mbadala inayopita kwenye eneo la wakwe zake kufika katika familia ya mjane huyo.

"Kwa sasa eneo hilo la makazi limerasimishwa kwa kuwa na mchoro wa Mipango Miji. Watu hao wameziba njia iliyokuwa inatumika kuanzia mwaka 2013, ambayo ipo kwenye ramani ya upimaji kwa kujenga nyumba mwaka jana."

Kutokana na ukatili huo, kiongozi huyo wa wilaya alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi wa eneo hilo kwenda na majembe kwa ajili ya kupasua barabara ya mita tatu, huku akishirikiana nao.

Aliagiza wataalamu wa ardhi kufanya marekebisho ya upimaji wa eneo hilo ili barabara iliyochongwa kwa kushirikiana na wananchi irasimishwe kisheria.

Vilevile, aliwataka wahusika waliomfanyia ukatili mjane huyo kuacha mara moja vitendo vya ukatili na unyanyasaji dhidi yake huku akiagiza vyombo vya dola kulinda usalama wa mjane huyo.

Pia alimtaka Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo kumkamata shemeji wa mjane huyo ambaye anatuhumiwa kuchochea mgogoro huo na kumfanyia mahojiano zaidi.

Akizungumzia mgogoro huo, mjane Rose alidai shemeji zake walimfungia njia na kuweka kaburi feki baada ya kukataa kurithiwa.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, akikata utepe kuzindua chumba cha vifaa vya ukalimani wa lugha mbalimbali katika Ofisi za Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ajali ya basi, lori yaua na kujeruhi

**Na Neema Hussein,** KATAVI

WATU wawili wamefariki dunia na tisa kujeruhiwa baada ya basi walilokuwa wakisafiria kugongana na lori la mizigo katika eneo la Unyenya wilayani Mpanda mkoani Katavi.

Ajali hiyo ilitokea juzi huku chanzo chake kikidaiwa kuwa ni mwendo kasi na uzembe wa dereva wa basi hilo wakati akijaribu kulipita lori hilo bila ya kuchukua tahadhari.

Akitoa taarifa ya ajali hiyo jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Benjamin Kuzaga, alisema waliopoteza maisha ni Rashidi Hamisi (30), mkazi wa Tabora ambaye ni utingo wa basi na Amani (18), mkazi wa Majimoto, Katavi.

Aliwataja majeruhi kuwa ni Omari Mohamedi (41), Suzana Gedion (47), Regina Faustine (41), Mwajuma Yusuph (30), Tatu Puli (3), Winfrida Michael (34), Neema Kapaliswa (32), Mariamu Luhende (42) na Tedson Mwambola (39).

Alisema kuwa baada ya ajali hiyo kutokea, dereva wa basi alikimbilia kusikojulikana na juhudi za kumtafuta kisheria bado zinaendelea.

Alisema miili ya marehemu imehifadhiwa Kituo cha Afya cha Mamba kwa uchunguzi zaidi wa kitabibu na majeruhi wanaendelea vizuri.

Kamanda huyo alitoa wito kwa wananchi na madereva katika mkoa huo kufuata sheria za usalama barabarani ili kuepusha ajali zisizo za lazima.

# Gwajima, Silaa matatani madai kulichafua Bunge

**Na Romana Mallya**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameamuru Mbunge wa Kawe, Josephat Gwajima (CCM), na Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa (CCM) kwenda mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kujibu tuhuma mbalimbali ikiwamo kusema uongo na kushusha hadhi na heshima ya Bunge.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa Ofisi ya Bunge, wabunge hao wanatakiwa kufika mbele ya kamati hiyo kwa mujibu wa Kanuni ya 4(1) (a) na (b) ya nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la mwaka 2020.



Silaa



Gwajima

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa kanuni hiyo inaipa mamlaka Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuchunguza mambo yanayohusu maadili ya wabunge yanayopelekwa kwa Spika.

"Mheshimiwa Gwajima anatakiwa kufika mbele ya Kamati ya Haki, Maadili ya Bunge Jumatatu saa saba kamili mchana katika ukumbi namba 229, jengo la utawala lililopo katika Ofisi ya Bunge Dodoma," inabainishwa katika taarifa hiyo ya Bunge.

Taarifa hiyo pia inamtaka Silaa kufika mbele ya kamati hiyo Jumanne saa 7:00 mchana katika jengo hilo ndani ya ofisi hiyo.

"Endapo yeyote kati ya waheshimiwa waliotajwa hawatafika mbele ya kamati kwa siku na muda uliotajwa, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa kifungu cha 17 na 34(1)(a) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge Sura ya 296 toleo la mwaka 2020," kunawekwa angalizo kwenye taarifa hiyo.




Katibu Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo, Ado Shaibu, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati akiiomba Serikali kuondoa tozo ya majengo kwenye Luku. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# ACT: Kodi majengo kwa Luku isitishwe

**Na Donald Lukele,** TUDARCo

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali kusitisha kukusanya kodi ya majengo kupitia mfumo wa ununuzi umeme njia ya Luku ili kutatua kwanza kero zilizoibuka kuhusiana na utaratibu huo mpya.

Kimesema baadhi ya wananchi watalipa kiwango kikubwa zaidi kutokana na nyumba wanazoishi kuwa na zaidi ya mita moja ya Luku.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema zipo baadhi ya nyumba ambazo mwenye nyumba huishi na wapangaji wake, hivyo kuwa na Luku zaidi ya moja na kwamba uhusiano wa mwenye nyumba na wapangaji haumwezeshi mpangaji kumwajibisha mwenye nyumba kutambulisha mita husika kwa Mamlaka ya Mapato (TRA).

"TRA inafahamu kuwa wenye nyumba wengi kwa vile hawaumizwi na kodi hii kwa wapangaji na kutokana na urasimu uliyopo serikalini, hawatapeleka mita husika TRA na wapangaji wataendelea kukatwa (kupitia) mita hizo," alisema Ado.

Alisema licha ya ufafanuzi wa TRA uliotolewa juzi kuhusu utaratibu huo kwamba wapangaji watakaokatwa fedha zao kimakosa, wawadai wamiliki wa majengo, bado kuna maswali mengi yanayokosa majibu.

Alisema serikali ilipaswa kwanza kabla ya kuanza kukusanya kodi kwa utaratibu huo, ifanye utambuzi wa Luku zinazopaswa kukatwa kodi hiyo ili kuepusha kukata watu kodi kimakosa.

Shaibu alisema sio vyema serikali kukimbilia kukusanya fedha bila kuweka mfumo mzuri wa ukusanyaji usio na dhulma.

Katibu Mkuu huyo katika mapendekezo ya chama hicho, alisema: "Serikali isitishe mara moja ukusanyaji wa kodi ya majengo kwa kutumia mita za Luku hadi hapo TRA itakapofanya utambuzi wa mita zinazostahili kukatwa kodi."

Pia alisema Bunge lifanye mapitio ya kodi ya majengo kupitia Luku na tozo ya miamala ya simu ili kuwaondolea mzigo mzito wananchi maskini na kutaka serikali itafute vyanzo mbadala vya kodi.

Mbali na suala hilo la ukusanyaji wa kodi ya majengo kwa Luku, Shaibu pia alisema mapambano ya kudai Katiba Mpya na Tume Huru ya Uchaguzi yanapaswa kuendelea ili uchaguzi uwe unatoa wawakilishi wa kweli wa wananchi ambao anaamini wasingekubali kupitisha sheria hiyo.

# Rais ateua Mnadhimu Mkuu JWTZ

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia suluhu Hassan, amemteua Meja Jenerali Matthew Mkingule, kuwa Mnadhimu Mkuu mpya wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Sambamba na uteuzi huo uliofanyika juzi, Rais pia amempandisha cheo na kuwa Luteni Jenerali. Amechukua nafasi ya Luteni jenerali Yacoub Mohamed aliyeteuliwa kuwa Baliozi wa Tanzania nchini Uturuki.

Jenerali Mkingule aliapishwa jana Ikulu jijini Dar es Salaam kushika wadhifa huo sambamba na wateule mbalimbali walioteuliwa na Rais hivi karibuni aliwamo Balozi Luteni Jenerali Yocoub.

Wengine walioapishwa sambamba na majenerali Yocoub na Mkingule ni Prof. Elisante Ole Gabriel kuwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama na mabalozi, Balozi Mahmoud Thabit Kombo (Italia), na Elsie Sia Kanza (Marekani).

Mbali na Jenerali Mkingule, wengine waliowahi kushika wadhifa huo ni Jenerali (mstaafu) Tumainieli Kiwelu, Luteni Jenerali (mstaafu) Martin Mwakalindile, Luteni Jenerali (mstaafu) Gideon Sayore na Luteni Jenerali (mstaafu) Iddi Gahhu.

Wanadhimu wakuu wengine ni Jenerali (mstaafu) Davis Mwamunyange, Luteni Jenerali (mstaafu) Abdulrahman Shimbo, Luteni Jenerali (mstaafu) Samweli Ndomba, Jenerali Venance Mabeyo na Luteni Jenerali (mstaafu) James mwakibolwa.

Akizungumza mara baada ya kuwaapisha viongozi hao, Rais Samia aliwataka kufanya kazi kwa bidii na kuwakumbusha kwamba wana majukumu makubwa na wamebeba matumaini ya Watanzania.

Rais Samia alimtaka Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Ole Gabriel kuhakikisha anasimamia maslahi ya watumishi wa Mahakama na kuhimiza utoaji wa haki na kufanya kazi kwa nidhamu na uadilifu.

Pia aliwataka mabalozi aliowaapisha kukuza na kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati ya Tanzania na nchi zingine pamoja na taasisi za kimataifa na kuwahimiza kulinda maslahi ya Tanzania kimataifa, kutetea maslahi ya Watanzania wanaoishi nje, kutafuta fursa za kibiashara, uwekezaji, utalii na ajira katika taasisi za kimataifa.

Hafla ya kuwaapisha viongozi hao ilihudhuriwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango; Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi; Waziri Mkuu Kassim Majaliwa; Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleimani Abdulla na viongozi mbalimbali wa serikali, vyama vya siasa, dini na mabalozi mbalimbali wanaowakilisha nchi zao hapa nchini.

**Rais Samia alimtaka Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Ole Gabriel kuhakikisha anasimamia maslahi ya watumishi wa Mahakama na kuhimiza utoaji wa haki na kufanya kazi kwa nidhamu na uadilifu.**

# Vurugu upandaji magari zashtusha

Na Costantino Michael, TUDARCo

KAIMU Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC), amewataka watumiaji wa huduma za usafiri ardhini kuacha tabia ya kugombania kupanda magari mjini.

Leo Ngowi amesema watumiaji wa usafiri huo wanapaswa kuwa na ustaarabu kwa kupanda magari kwa kupanga mstari, jambo ambalo litasaidia kwa kiasi kikubwa kuleta mabadiliko kwenye Sekta ya Usafirishaji nchini.

Alitoa rai hiyo jana alipozungumza na Nipashe, akisema ni wakati mwafaka kwa abiria kurejea kwenye ustaarabu na kuacha kufikiri kuwa kuingia kwenye vyombo vya usafiri kwa fujo ni tabia ya kawaida.

Ngowi alikumbusha baada ya Uhuru wa nchi, kulikuwa na ustaarabu hasa abiria kupanda magari kwa kupanga mstari lakini baada ya mwaka 1984, nchi ilipoingia kwenye soko huria, mambo yaliharibika na ustaarabu ukaanza kuondoka na sasa kunashuhudiwa abiria wanaingia kwenye magari kwa fujo.

Aliongeza kuwa baraza limeona ni vizuri sasa kuja na mpango wa kitaifa kuhamasisha jamii kupanda kwenye magari kwa kupanga mstari na kwa kuanzia watatoa elimu ya falsafa ya kubadilisha tabia katika eneo hilo.

Kiongozi huyo alisema mkakati wao huo utawahusisha moja kwa moja madereva, makondakta, wamiliki wa vyombo vya usafiri, Jeshi la Polisi, LATRA na vyombo vya habari.

Ngowi alitaja madhara ya watu kupanda magari kwa fujo kama vile watoto kuathirika kisaikolojia, wazee na kinamama wajawazito kupata matatizo ya kiafya, watu wenye ulemavu na mahitaji maalum kukosa haki ya kuingia kwenye vyombo vya usafiri, kujeruhika, kuibiwa, kuambukizana magonjwa, kuondoa unadhifu wa mtu na wakati mwingine hata kusababisha udhalilishaji wa utu wa mtu.

**Mkakati wao huo utawahusisha moja kwa moja madereva, makondakta, wamiliki wa vyombo vya usafiri, Jeshi la Polisi, LATRA na vyombo vya habari.**

# Walimu madrasa matatani kipigo kikali kwa wanafunzi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imesema inakusudia kuunda kamati maalum kuchunguza tukio la udhalilishaji na kupigwa kupita kiasi kwa wanafunzi wa Shule ya Suni Madrasa iliyoko mjini Unguja kunakodaiwa kufanywa na baadhi ya walimu wa shule hiyo.

Akitoa taarifa maalum kwa waandishi wa habari wizarani kwake Mazizini jana, Waziri Simai Muhammed Said alisema wizara imejiridhisha kuwa tukio hilo ni la kijinai lisilopaswa kufanywa na walimu na kamwe haitavumilia kuona walimu wa aina hiyo wanafanya matukio ya ajabu dhidi ya wanafunzi.

Akizungumza kwa masikitiko baada ya kuangalia video ya udhalilishaji uliofanywa na baadhi ya walimu hao ambao chanzo chake ni baadhi ya wanafunzi kunyoa nywele zao kwa mtindo wa kiduku, alisema jambo hilo ni kinyume cha sheria, sera na kanuni ya wizara hiyo katika utoaji wa adhabu mbadala.

Waziri Simai alisema wizara iko kwa ajili ya kuwalinda wanafunzi, ushauri kwa walimu na msaada wa kisheria pale shida zinapojitokeza.

Alisema walimu wa shule hiyo walipaswa kufika wizarani kupata ushauri badala ya kujichukulia sheria mikononi kuwaadhibu wanafunzi.

Alisema inaunda kamati ili kuchunguza umiliki wa shule hiyo, bodi ya shule na walimu wa shule hiyo.

Waziri huyo pia alisema amesikitishwa na tamko la Chama cha Walimu Zanzibar kuhusu hatua iliyochukua wizara, akisisitiza ilipaswa kuonana na wizara kabla ya kutoa taarifa bila kuangalia video ya tukio hilo.

Alisema wizara anayoiongoza inakusudia kuzifanyia tathmini ya leseni zote katika shule binafsi ambazo nyingi zimepitwa na wakati pamoja na viwango vya elimu vya walimu wa shule hizo.

Alizitaka shule binafsi kufahamu kuwa zipo chini ya usimamizi wa wizara na zinapaswa kufuata Sheria ya Elimu Na. 6 ya Mwaka 1982 iliyofanyiwa marejeo mwaka 1993 kuhusu kanuni na mwongozo wa uendeshaji wa shule binafsi.

Mrajis wa Elimu, Zuwena Mataka, alisema shule nyingi hazifuati miongozo ya utoaji wa adhabu mbadala kwa wanafunzi ikiwamo upigaji wa viboko.

Alizitaja adhabu hizo kosa la kwanza mwanafunzi hutakiwa kupewa onyo, kosa la pili onyo kwa maandishi na hatua ya mwisho endapo wanafunzi atarejea kosa ni kumsimamisha masomo na sio kumpa kichapo kikali.

Waziri Simai alilazimika kiwaonyesha video ya udhalilishaji uliofanywa na baadhi ya walimu wa shule hiyo dhidi ya wanafunzi wao baada ya kuenea taarifa katika mitandao ya kijamii kuwa kitendo alichokifanya kuwasimamisha kazi walimu hao ni uonevu.

Hatua hiyo imejiri baada ya wazazi wa wanafunzi waliopata kipigo kutoka kwa walimu wao, kulalamika kuhusu kadhia hiyo.




Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, akijaribu pikipiki iliyotolewa na Hoteli ya Ramada Resort by Wyndham, baada ya kuzindua kituo kipya cha Polisi Jangwani Beach, kilichojengwa na hoteli hiyo kwa thamani ya Sh. milioni 25 katika Mtaa wa Kilongawima, Kata ya Kunduchi, mkoani Dar es Salaam jana. Kulia ni Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, ACP Muliro Jumanne na Mkurugenzi wa Fedha wa hoteli hiyo, Saleem Aboonhi. **PICHA: JOHN BADI**

# COSTECH yawapa mbinu wabunifu

Na Renatha Msungu

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imewataka vijana wabunifu walioko kwenye kampuni changa kutobweteka na kuridhika na kile walichonacho badala yake waendelee kudadisi na kujifunza ili wapige hatua.

Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, alitoa rai hiyo alipozungumza na vijana kutoka kampuni changa kwa lengo la kupata washindi wawili watakaokwenda kushiriki kwenye mashindano ya kimataifa kwa ajili ya kutoa mawazo yao kuona kama yanaweza kufadhiliwa na kupata mafunzo zaidi.

Dk. Nungu alisema wanapanga kusaidia vijana mafunzo ya kwenda Finland na pia kushindanisha kampuni changa kwa ajili ya kutoa huduma zao katika washirika.

Alifafanua zaidi kuwa vijana wengi walioko katika kampuni hizo wanakuwa na mawazo ya kuchangia kujenga uchumi wa viwanda nchini ndiyo maana tume inawakusanya kwa pamoja ili kuendeleza mawazo yao.

Mkurugenzi huyo alisema katika mchakato huo wamepokea maombi 79 na wamefanya mchujo na kubakia kampuni chache ambazo zitashindanishwa na kupatikana kwa washiriki wawili.

"Tulifanikiwa kupata kampuni zaidi ya 10 ambazo ziliweza kushindana na kushinda kwa kupata ufadhili kwa kushirikiana na wenzao.

"Katika hilo tunajivunia Kampuni ya Arusha na Filter ambao wao walipata ufadhili wa kupeleka teknolojia yao Zambia kupitia mradi huu wa SAIS.

"Katika miradi hiyo zaidi ya 10, miwili ilikuwa inalenga kusaidia vijana wa kike na kinamama kushiriki katika masuala ya TEHAMA," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema mchakato huo upo chini ya Mradi wa Kukuza Ubunifu Kusini mwa Afrika (SAIS) ambao nchini COSTECH ndiyo msimamizi wake.

Dk. Nungu alisema mradi huo unafadhiliwa na Serikali ya Finland na ulianza mwaka 2017 ukijumuisha Tanzania, Botswana, Msumbiji, Namibia, Afrika Kusini, Zambia na nchi wanachama wengi wa SADC, lengo likiwa kujenga mifumo ya ubunifu ndani ya nchi zilizo katika mradi huo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kukemea kukatika umeme haitoshi, wahusika wapewe adhabu ili kumaliza tatizo

**WAZIRI** wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, juzi alitoa kauli juu ya kukatika mara kwa mara kwa umeme katika maeneo mbalimbali yakiwamo Dar es Salaam na Dodoma na kuwapiga marufuku maofisa na wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) juu ya tabia hiyo.

Katika kukemea tabia hiyo, Waziri Kalemani alisema kisingizio kikubwa cha wafanyakazi kukatika kwa umeme ni kuhamisha gridi ya taifa. Aliweka bayana kwamba tabia inakera kutokana na baadhi ya watendaji wa TANESCO kukata umeme bila kutoa taarifa.

Akitolea mfano wa Dodoma, alisema serikali ilishapiga marufuku kukatwa ovyo kwa umeme kutokana na kuwa ndiko makao makuu ya serikali lakini inashangaza kuona tabia hiyo bado inaendelea. Hakuishia hapo tu bali alionya kwamba tabia hiyo itamwondoa mtu kwenye nafasi yake.

Pamoja na kusema hayo, Waziri alibainisha kuwa umeme katika Mkoa wa Dodoma kwa sasa ni wa kutosha kutokana na kuwapo kwa kituo cha kufua umeme cha Zuzu ambacho kinatarajiwa kukamilika Septemba 27, mwaka huu, na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha zaidi ya Megawati 600 za umeme.

Licha ya kutangaza juzi kuwa ni marufuku kwa tabia hiyo kuendelea, tatizo la kukatika kwa umeme, kwa Mkoa wa Dar es Salaam mathalan, limekuwa sugu. Hoja kubwa inayotolewa ni kubadilisha nguzo za umeme kutoka za zamani za miti kwenda za zege ambazo zinadumu kuliko zile za awali.

Tabia hiyo ya kukatwa umeme takriban kila siku kwa maeneo kama Tabata, Segerea, Mikocheni, Mwenge, Ubungo, Kinyerezi na Ukonga imekuwa kero kubwa. Kwa wastani, wananchi wa maeneo hayo, zaidi ya mwezi sasa, wanakatiwa umeme bila taarifa. Wakati mwingine unaweza kukatika na kurejea baada ya muda mfupi jambo ambalo linaweza kusababisha wananchi kupata hasara ikiwamo kuunguliwa kwa vyombo vinavyotumia umeme.

Hivi sasa katika maeneo hayo na mengine hasa ya kibiashara kama Kariakoo, katikati ya jiji la Dar es Salaam na Mwenge ambako umeme unahitajika kwa wingi kwa ajili ya uzalishaji, kumeshamiri kelele za majenereta kutokana na kadhia hiyo ya kukatika kwa umeme mara kwa mara.

Kwa ujumla umeme ni nishati muhimu kwa maisha ya kila siku ya Mtanzania na mwanadamu awaye yote kutokana na umuhimu wake hasa kwa shughuli za uzalishaji mali hata zile za nyumbani. Kwa mantiki hiyo, unapokatika unasababisha usumbufu mkubwa ikiwamo kupungua kwa uzalishaji mali au watu kuamua kutumia majenereta ambayo matumizi yake ni ya gharama kubwa.

Kauli aliyoitoa Waziri Kalemani kuhusu tabia iliyozoeleka miongozi mwa watendaji wa TANESCO ya kukata umeme ovyo, ni ya kuungwa mkono kwa sababu ina athari kubwa kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Tunasema ni ya kuungwa mkono kwa sababu wananchi wamechoka na tabia hiyo hasa kutokana na athari wanazozipata kwa vitendo hivyo.

Pamoja na kuunga mkono, kauli pekee haitoshi bali vinatakiwa vitendo kwa kuchukuliwa hatua dhidi ya wahusika na kuwa funzo kama ambavyo Waziri alichukua hatua hivi karibuni kwa kuwaondoa kwenye nafasi baadhi ya mameneja wa TANESCO na wahandisi kutokana na kushindwa kutimiza malengo katika usambazaji umeme vijijini.

Kimsingi, maneno juu ya kuwataka watendaji wa taasisi mbalimbali kubadilika na kuacha kufanya kazi kwa mazoea, ikiwamo kwa watumishi wa TANESCO, ni wimbo uliozoeleka masikioni mwa Watanzania. Kinachotakiwa sasa ni hatua dhidi ya wanaorudisha nyuma jitihada za serikali, ikiwamo kuwaondoa kwenye nafasi zao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kilimo cha kisasa kinaweza kuchagiza uchumi viwanda



Na Sabato Kasika

**KILIMO** cha kisasa nchini, bado kina mwendo wa kusuasua tangu Tanzania ilipopata Uhuru, wakulima wengi wanatumia jembe la mkono, ambalo uzalishaji wake hauwezi kuleta tija kama wangetumia nyenzo za kisasa.

Teknolojia na nyenzo mbalimbali za kisasa yakiwamo matreka, vinaweza kumsaidia mkulima kuboresha kazi yake kwa kulima eneo kubwa kuliko jembe la mkono ambalo humfanya achoke mapema.

Hivyo, ili kuchagiza Tanzania ya viwanda, ambayo kwa namna moja au nyingine inategemea mazao ya kilimo, nadhani ni muhimu kuweka mikakati ya kuhakikisha Mtanzania inaachana na kilimo cha kutegemea jembe hilo.

Si kuachana na jembe hilo tu, bali pia kama inawezekana, basi mkulima pia asaidiwe kuachana na kilimo cha kutegemea msimu wa mvua, ambao kutokana na mabadiliko ya tabianchi anaweza kujikuta anakosa mavuno.

Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Tanzania ililenga kuifikisha Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati kupitia sekta ya viwanda ifikapo mwaka 2025, ambapo inakusudia kubadili uchumi wa Tanzania kutoka kutegemea sekta.

Sekta ya kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania, ingawa tija ndogo kutokana na kwamba wakulima wengi wanategemea jembe la mkono ambalo uzalishaji wake shambani ni mdogo. Kwa kuwa tunataka kuwa taifa lenye kutegemea zaidi uchumi wa viwanda na hasa viwanda vyenye kutengeneza bidhaa zenye ubora wa kumudu ushindani wa soko la kimataifa, ni vyema kuwekeza kwenye kilimo pia.

Viwanda vinaweza kujengwa vingi, lakini uzalishaji shambani ukawa duni kutokana na zana za kilimo, hasa jembe la mkono, lakini kikiboreshwa kutoka cha zamani kuwa cha kisasa kitasaidia kuwa na Tanzania ya viwanda.

Ikumbukwe viwanda vinategemea mazao mbalimbali kutoka shambani kama mahindi, mtama, mihogo, karanga, korosho, tumbaku, kahawa, ufuta, mpunga, mahindi na katani.

Ili uzalishaji uwe wa kutosha, ninadhani ni muhimu kuachana na kilimo cha jembe la mkono na kwenda cha kisasa ili kama nchi inakwenda kuwa ya viwanda, basi uzalishaji shambani nao uwe mkubwa.

Kama inashindikana kutoka jembe la mkono hadi kilimo cha kutumia trekta, si vibaya kutumia hata cha jembe la kukokotwa na ng'ombe, ambalo kwa kiasi fulani lina unafuu kwa kulima sehemu kubwa ya shamba kuliko la mkono.

Ninatambua kuwa kwa sasa, yako baadhi ya maeneo ambayo wadau wa kilimo wameamua kuhamasisha wananchi wake kuelekeza nguvu katika kilimo cha jembe la kukokotwa na ng'ombe ili kupanua shughuli zao.

Hatua hiyo kwa mtazamo wangu ni inaweza kusaidia wakulima kutumia muda mfupi kulima eneo kubwa la shamba na kama hali ya hewa inakuwa nzuri wanaweza kupata mavuno mengi kuliko jembe la mkono.

Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, ni miongoni mwa wadau hao wanaohamasisha kilimo hicho kwa kugawa bure majembe ya kukokotwa na ng'ombe kwenye vikundi vya wakulima.

Mwenyewe anasema huo ni mkakati wa kumtua mkulima jembe la mkono kwa kuanzia kwenye plau huku mikakati kuwasiliana na halmashauri ili kukopesha wakulima fedha za kununua trekta zikiendelea.

Kimsingi, mbinu hiyo ikitumiwa na wadau wote wa kilimo kwenye maeneo mbalimbali nchini, inaweza kusaidia angalau kuwezesha wakulima kupanua mashamba na hata kuwezesha Tanzania ya viwanda.

Kwa kuwa ni vigumu kila Mtanzania kutumia trekta, lakini siyo vibaya kuanzia kwenye kilimo cha kutumia jembe la kukokotwa na ng'ombe (plau) wakati maandalizi ya kwenda kwenye kilimo cha kutumia trekta yakiendelea.

Uhamasishaji huo wa kuanzia kwenye plau unaweza kuwa ni dalili za kumtua mkulima jembe la mkono kuelekea kwenye trekta, ili naye aonekane wa kisasa kuliko kuendelea kulima kizamani.

Si rahisi kutenganisha Tanzania ya viwanda na kilimo, kwani vyote vinategemeana, hivyo ingependeza uboreshaji wa kilimo nchini kutoka jembe la mkono kwenda mbele ungepewa msisitizo.

Hatua ya kugawa plau inaonyesha mwanzo mzuri kuelekea kwenye kilimo cha trekta, ambacho kimsingi kinaweza kuwa na manufaa kwa Tanzania ya viwanda kuliko jembe la mkono.

**SAFU**

**FIKRA MBADALA**



Pascal Mayalla

# Chanjo ni hiari chonde chonde tusiwatishe wale wanaopinga

KWA vile chanjo ni hiari, tusitumie vitisho dhidi ya wanaopinga. Tutumie elimu kuwaelimisha Watanzania umuhimu wa chanjo, elimu kuhusu chanjo na faida za chanjo, ili kupata uhiari wao.

Wakati huo huo, elimu hiyo ya chanjo, itawafanya wapinga chanjo wenye hoja kujibiwa kitaalamu, hivyo wapinga chanjo wajinga, kuonekana ni wajinga tu na hatimaye Watanzania kuwapuuza kwa kuonekana wanapinga chanjo kwa ujinga tu wa kutojua. Wakielimishwa, ujinga utawatoka na wataikubali chanjo na kuwahimiza wafuasi wao wakachanje.

Kati ya wapinga chanjo, kuna wapinga chanjo wa aina mbili. Wako wale wenye hoja na wapinga chanjo wajinga wenye hoja. Hawa hoja zao zijibiwe. Lakini kuna wapinga chanjo wapumbavu, hawa wapuuzwe.

Wapinga chanjo wajinga, hawa wanapinga chanjo kwa ujinga tu wa uoga wa kutokujua kitu kilichomo ndani ya chanjo, inafanyaje kazi na matokeo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ni nini. Hawa wasitishwe, bali waelimishwe tu na ujinga utawatoka, wataikubali chanjo.

Mjinga akielimishwa, ujinga mnamtoka na anakuwa mwerevu. Lakini mjinga ambaye ameelimishwa, haelimishiki na bado anaukumbatia ujinga, huyu sasa si mjinga bali ni pumbavu. Hata aelimishwe vipi, ataendelea kupinga tu. Kuendelea kumwelimisha mtu kama huyu, ni sawa na kumpigia mbuzi gita. Dawa pekee ya kumsaidia mtu wa aina hii ni kumpuuza.

Hivyo kuna wapinga chanjo wajinga na kuna wapinga chanjo wapumbavu. Mpinga chanjo mjinga ni mtu mwenye akili zake timamu ila amekosa tu elimu ya kujua kuhusu chanjo ndiyo maana naisisitiza serikali yetu ijikite kwenye kutoa elimu ya chanjo ili kuwaelimisha Watanzania kuhusu chanjo na kupata ridhaa yao kupitia kuwa na kitu kinachoitwa 'informed decision'.

Lakini wapinga chanjo wapumbavu, hawa ni 'attention seekers', wanapinga chanjo kwa sauti kubwa si kwa lengo la kupinga chanjo, bali kutafuta wafuasi wa kuendelea kutunisha makusanyo.

Serikali yetu inapotumia vitisho na kumtumia mtu jeshi la polisi kumkamata, huku ndiko kumpatia anachotaka. Kama jeshi letu la polisi, litamkamata kweli na kumhoji, huku ni kumpatia umaarufu alioutaka.

Matokeo yake, ni watu wengi zaidi watamwamini na kuogopa chanjo kwa hoja kuwa kama chanjo ni hiari, wahamasishaji tu ndio wenye hiari halali. Lakini wapinga chanjo wanakamatwa na polisi, hivyo wataamini ni kweli kuna jambo linafichwa.

Wenzetu wazungu, wana msemo wa Kiingereza, "never argue with a fool, people may not notice the difference". Kwa Kiswahili ni usibishane na mpumbavu, watu watashindwa kutofautisha.

Pia kwa Kiswahili, pia tuna msemo kwamba ukiwa unaoga mtoni, huku nguo zako zote umezivua, akatokea kichaa akazichukua nguo zako na kuanza kukimbia nazo na wewe ukaamua kutoka hivyo ulivyo na kuanza kumkimbiza, mtaani hakuna atakayetofautisha nani ni kichaa na nani ni mzima! Hivyo unashauriwa ukiwa unaoga mtoni, ukaibiwa nguo na kichaa fulani, unachopaswa kufanya ni kuchutama, mpaka utokee msaada.

Kwenye huu uhiari wa chanjo, kuna vichaa fulani wanaivua nguo serikali yetu kwa kupinga chanjo. Baadhi ya vichaa hawa ni viongozi wa serikali yetu ambapo wana mamlaka zao za nidhamu ambazo ndizo zingepaswa kuwashughulikia tangu mwanzo walipoanza mdogo mdogo.

Kitendo cha serikali yetu kuwatishia kwa polisi, mara waziri akijibishana kwa lugha zile zile za mtaani za kuvuana nguo na kudhalilishana kama kuitana "kibwetere", "kufufua wafu", "mkono wa bauncer" na "kutesti mitambo", mara kuliagiza jeshi la polisi na Takukuru "kama huyu" wakati mamlaka hayo hawana, mara Afande IGP anajibu, na labda Jumapili ya leo "ataliamsha dude", hazijengi wala hazihamasishi chanjo wala watu kujitokeza kuchanja. Dawa pekee ya kuhamasisha chanjo na kupata uhiari wa Watanzania, ni kuotoa elimu ya chanjo.

***Pasco Mayalla***
***pascomayalla@gmail.com***
***Mob. +255 754 270403***

**MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO**



Na Joseph Kulangwa

# Mtifuano Gwajima na Gwajima hapatoshi!

BINADAMU, mnyama na viumbe wengine hai, huzaliwa na kukua na tabia tofauti. Kimsingi hubadilika kadri wanavyokua na huendana na mabadiliko ya mazingira.

Mtu uliyekutana naye miaka takribani mitano iliyopita, usishangae kumwona amebadilika tabia na kuwa tofauti. Anaweza kuwa mkali au mpole kupindukia, kutokana na mapito aliyopitia.

Watanzania walioishi ulimwengu wa Dk. John Magufuli kuanzia mwaka 2015 mpaka anafariki dunia mwanzoni mwa mwaka huu, si wanaoishi ulimwengu wa Rais Samia Suluhu Hassan, aliyerithi mikoba ya JPM.

Watu waliopokea UVIKO-19 mwaka juzi, sivyo walivyopokea wimbi la ugonjwa huo mwaka huu, baada ya JPM. Mwaka juzi na mwaka jana, walikuwa wakiamini katika kuishinda korona kwa maombi.

Walioamini katika kuishinda kwa kutovaa 'mabarakoa' na kutoamini kabisa katika kujifungia majumbani ili kukabiliana na ugonjwa huo hatari, waliwacheka sana waliovaa 'mabarakoa' yao.

Binadamu hao hawakuamini kabisa katika chanjo, wakisema haiwezekani kutafitiwa, kugundulika na kuanza kutumika ndani ya mwaka mmoja, wakisema chanjo imewahi, sana sana ilihitaji miaka 10, wakaamini katika unywaji mchanganyiko wa matunda machungu na yenye ugwadu na nyungu.

Lakini baada ya JPM kutangulia mbele za haki, ni hao hao, ambao leo hii wanaamini katika 'mibarakoa', wanaamini katika chanjo na wanaamini kwamba kujifungia ni halali, ingawa katika nchi masikini kama Tanzania ni shughuli pevu.

Ukifuatilia na ukawahoji kisa cha kubadilika msimamo, watakujibu haraka sana, kwamba kila zama na kitabu chake. Nawe ukiongeza za mbayuwayu, utaelewa kuwa wengi waliangalia wanamtumikia nani wakati huo, na sasa wanamtumikia nani.

Unaweza kuja na jibu rahisi tu, kuwa tumbo kwanza kichwa baadaye katika kila kitu. Kwamba ukiendekeza kichwa muda mrefu, utajikuta unaumiza tumbo, ambalo litakaa tupu muda huo na matokeo yake kuwa mabaya.

Hii kitu chanjo ya Uviko-19, imeleta mambo mengi na ya kustaajabisha sana. Tunashuhudia malumbano ya hadharani tena yakihusisha watu wazito ambao ndio wa kutuonesha mifano nasi tukaiga.

Rais Samia alipoingia madarakani na kuangalia nchi yake inavyokwenda, akakubali kuunda kamati ya kumshauri kuhusu Uviko-19, ilipompa taarifa baada ya kuchunguza mazingira na makandokando ya ugonjwa huo, akakubali chanjo iletwe.

Akakubali nchi kujiunga na mpango wa Covax, tukaletewa dozi ya Jenssen kutoka kampuni ya Johnson & Johnson ya Marekani. Akachanjwa, nasi tukachanjwa. Ghafla kiongozi wa kundi fulani la imani, akaibuka na kuzomea, akikataa kuchanjwa akakataza na 'familia' yake sawia.

Askofu Josephat Gwajima wa Kanisa la Uzima na Ufufuo, akashikilia msimamo kila Jumapili akihubiri familia yake madhabahuni, bila utafiti wa kisayansi, akasema wachanjwao wanaingizwa madude miilini ambayo itawaua.

Kumbe katika mahubiri yake, akatamka kuwa kuna watu wameshikishwa kitu kidogo ili chanjo iletwe kutuua. Nani sasa kashikishwa? Rais au shemeji yake, Dorothy Gwajima, Waziri wa Afya, ambaye ni mke wa Methusela?

Askofu Josephat hakuchoka, kila alipopata wasaa akahanikiza pingamizi, huku akijua kabisa kuwa chanjo ni hiyari, lakini akakomaza mishipa ya shingo kuponda. Hatimaye Dorothy uvumilivu ukamshinda dhidi ya shemela wake.

Akaitisha wenye vyombo vya ulinzi na usalama, wamweke mtukati shemela, ili abaelezee na kutoa ushahidi wa tuhuma zake kwa Mkuu wa nchi na yeye mwenyewe mama watoto wa Methusela. Dorothy akafunguka mpaka ya marehemu Amina Chifupa na yule Mkono wa Baunsa!

Kwa kweli sikutarajia, kwa sababu kwa uhusiano ule wa kinasaba, nilitarajia Dorothy angerejea kanuni ya 'mgongano wa kimaslahi', asimseme vile shemela wake, na badala yake angemwachia hata mdogo wake, Mollel akayasema hayo.

Lakini hakujali, yalimfika shingoni, kumsema anayewezesha kono lake kwenda kinywani, wee!

Josephat naye alivyosikia shemela kamwaga mboga, naye akasema subirini Jumapili (leo) nimwage ugali! Nimjuavyo Josephat, haki ya nani mshale umechomoka kunako upinde, tusubiri utakakotua utaacha madhara gani! Nimekumbuka yale na Bashite enzi zile! Kama namwona Methusela Jumapili hii! Yetu masikio, tuchokonoe nta tu, tusikie yajayo! Alamsiki!

KONA YA UKWELI

# Malalamiko ya wenye ulemavu yasipuuzwe na Jeshi la Polisi



Na Thobias Mwanakatwe

AGOSTI 11, mwaka huu, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kiliandaa kikao kazi kwa mawakili wabobezi na viongozi wa vyama vya wenye walemavu kwa ajili ya kuichambua Sheria ya Usalama Barabarani Na. 168 ya mwaka 1973.

Lengo la kuichambua sheria hiyo na kanuni zake lakini Ofisa Programu kutoka LHRC, Joram Bwire, alisema ni kwa kwa sababu sheria hiyo haiweki bayana ulinzi kwa watu wenye ulemavu ambao nao ni watumiaji wa barabara, hivyo kusababisha wapate ajali mara kwa mara.

Katika kikao hicho, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Jonas Lubago, alisema Sheria ya Usalama Barabarani ipo kimya juu ya watumiaji barabara wenye ulemavu wa aina mbalimbali. Hali hiyo, alisema inasababisha changamoto na kuleta madhara mengi na hata kupoteza maisha.

Akasema watu wenye ulemavu wengi wamekuwa wakigongwa na magari, pikipiki na bajaji kutokana na madereva kutojua jinsi ya kutoa ushirikiano kwa watumiaji wa barabara hasa wenye ulemavu.

Lubago akasema sheria hiyo haitoi mkazo mahususi kwa kuzieneza alama za barabarani za watu wenye ulemavu na pia alama hizo hazitambuliki na sheria na hakuna hata dereva mmoja aliyewahi akufundishwa kwenye vyuo vya udereva.

Aliongeza kuwa hata alama za barabarani za walemavu zilizopo, serikali kupitia mamlaka husika haijazisimika kwenye maeneo yanayohitajika hali ambayo inasababisha ajali nyingi zinazohusisha walemavu.

Lubago pia alisema Sheria ya Usalama Barabarani inatakiwa kuainisha aina na viwango vya magari yanayotoa huduma ya usafiri wa umma ambavyo ni pamoja na uwepo wa milango mipana ya mabasi, nafasi ya kupita na kiti mwendo katika korido na nafasi kati ya kiti na kiti inayoruhusu mtu mwenye ulemavu kuketi.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, Sheria ya Usalama Barabarani lazima itoe mwongozo wa uwepo wa maegesho mahusui kwa magari kwa watu wenye ulemavu. Mfano, unapokwenda kwenye kituo cha daladala au mabasi, je, kuna maegesho mahususi kwa walemavu ambayo hayaingiliwi?

Kwanza nianze kwa kuipongeza LHRC kwa kuona umuhimu kwa watu wenye ulemavu kuwapa fursa hiyo muhimu ya kuichambua sheria hiyo ili mamlaka zinazohusika zichukue hatua. Pili, niwapongeze watu wenye ulemavu ambao walitumia muda wao kuipitia sheria hii na kutoa mapendekezo kwa serikali nini kifanyike ili kuwalinda walemavu wasiendelee kupoteza maisha.

Natambua kuwa moja ya majukumu ya Jeshi la Polisi ni pamoja na kulinda raia ili wabaki salama. Raia hao wanaozungumzwa ni pamoja na watu wenye ulemavu.

Watu hao katika kikao kazi hicho utaona wamelalamikia sana sheria hiyo kutowajali. Sitashangaa kusikia malalamiko kama haya pengine wamekuwa wakiyatoa kila mara na kuyawasilisha kwa mamlaka za serikali zinazohusika lakini hayafanyiwi kazi.

Nitoe masikitiko yangu kwamba mamlaka nyingi inapofikia suala la walemavu zimekuwa hazioni umuhimu wa kutatua changamoto zinazoikabili jamii hiyo na hii imekuwa ni kama kasumba fulani.

Wanaohusika katika mamlaka hizo likiwamo na Jeshi la Polisi lazima watambue kuwa sisi sote ni watu wenye ulemavu watarajia hivyo tunaposhindwa kutatua changamoto zao ipo siku na sisi tutakuwa walemavu.

Kwa hiyo ifike hatua, wenye ulemavu wanapohitaji ombi lao basi mamlaka husika wasipuuze kwasababu wao hawakuomba wawe hivyo ni mipango tu ya Mwenyezi Mungu.

Tuheshimu haki zao, tuwalinde na tuwajali kwa sababu na wao ni binadamu kama wengine. Tunaposhindwa kutatua changamoto zao, tujue tunamuudhi hata Mwenyezi Mungu aliyetuumba sisi sote.

Ni matumaini yangu kwa kuwa suala la kusimania Sheria ya Usalama Barabarani lipo chini ya Jeshi la Polisi, mapendekezo yaliyotolewa na walemavu kuhusu sheria hiyo yatafanyia kazi.

***Mungu libariki Jeshi la Polisi, Mungu wabariki walemavu.***

***Kwa maoni tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com***

DARASA LA NDOA

# Matumizi ya simu yanayoathiri uhusiano baina ya wanandoa - 2



Na Mch. Dk. Enock Mlyuka
0744000066

BAADHI ya wanandoa wamekuwa watumwa wa simu zao. Wengi pia hawana nidhamu ya matumizi ya simu zao. Hawajui mahali na wakati unaofaa au usiofaa kutumia simu.

Imetokea mahali pengine kwamba, mke na mume wakiwa katika mapumziko ya pamoja, matembezi, faragha au nyumbani, kila mmoja au mmoja wao anakuwa amezama katika simu yake muda mwingi kuliko kupata muda na mwenzi wake. Mwenzi anajali zaidi simu yake kuliko uhusiano wake na mumewe au mkewe, hivyo, kuwa mtindo wa maisha. Simu ya mkononi imekuwa kama mke au mume wa pili.

Simu ya mkononi ni chombo binafsi cha mawasiliano na sheria ya mawasiliano nchini inamlinda mtumiaji. Mtu anaposajili simu au kadi ya simu (line), atasajili kwa jina lake binafsi kwa kutumia kitambulisho chake cha taifa na kuweka alama za vidole vyake. Kwa mantiki hiyo, yeye ndiye muhusika mwenye dhamana na simu au kadi hiyo.

Pale litakapotokea tatizo kuhusiana na simu hiyo, atakayewajibika ni mwenye simu hiyo. Kwa kuwa simu ya mkononi ni chombo binafsi cha mawasiliano, ni wazi kuwa simu imejaza taarifa nyingi binafsi za mtu. Mume au mke kutamani kupekua pekua simu ya mwenzi wake ni kumkosea kwani kufanya hivyo ni kuingilia uhuru wa mtu mwingine katika matumizi ya simu yake. Hii ni dalili ya wanandoa kutokuaminiana.

Mwanadamu hachungwi bali anajichunga na kulindwa na Mungu. Ni dhahiri kuwa tabia ya mke au mume kufuatilia kilichomo kwenye simu ya mwenzi wake ili kujua anawasiliana na watu wa aina gani ni dalili ya kutojiamini, kutokukua na kutokomaa katika uhusiano.

Kama kuna tatizo, kwa vyovyote, hiyo huwa si njia nzuri ya kushughulikia tatizo. Kufanya hivyo ni sawa na kushughulika na dalili za ugonjwa (symptoms) badala ya kushughulika na kiini chake (source). Ni busara wanandoa wakatambua kwamba, mara zote tatizo si yale yaliyomo katika simu, bali tabia binafsi ya mtu huwa ndio kiini cha tatizo. Kwani watu wengine wana tabia mbaya zinazotokana na makuzi na malezi wakati wa utoto.

Kufuatilia simu ya mwenzi wako na kutilia shaka kila mawasiliano anayofanya, hakutasaidia kutatua tatizo. Zaidi sana kutaongeza ukubwa wa tatizo na kusababisha ugomvi na kukuletea msongo wa mawazo usio wa lazima na kukufanya uishi maisha yenye hofu. Hali ya namna hii ni hatari katika maisha ya mtu, kwani huathiri afya ya mwili na akili hata kuweza kusababisha kifo.

Siku zote, mjenzi na mbomoaji wa ndoa ni mwanandoa mwenyewe. Matatizo mengine yametokea katika baadhi ya ndoa pale ambapo mke au mume analazimisha kutaka kujua taarifa zilizomo kwenye simu ya mwenzi wake bila utayari wa mwenzake. Matokeo yake ni ugomvi na kuumizana. Ndugu mwanandoa, kasoro zinapojitokeza zinaweza kumalizwa kwa mazungumzo na siyo kupigana.Wanandoa wajifunze kupenda kuzungumza, kwani si kila tatizo wanaweza kusaidiwa na watu wengine.

Ndoa bora hujengwa na mawasiliano imara. Wanandoa wajenge utamaduni wa kuzungumza na kuulizana kwa upole kama kuna jambo ambalo wanaona haliko sawa katika matumizi ya simu zao. Kukasirika, kususa, kuzungumza lugha mbaya na kuumizana haitasaidia, bali kutachochea ugomvi.

Yamkini changamoto inaweza kuwapo katika mawasiliano, lakini namna inavyoshughulikiwa inaweza kuleta tatizo, kwani tatizo la watu wengi ni kutokujua namna ya kushughulikia tatizo linapojitokeza. Kwa hiyo wanandoa wajifunze kuwa watulivu tatizo linapojitokeza ili kutafuta njia sahihi ya utatuzi wake. Maneno ya Mungu yanasema "Azuiaye maneno yake ni mwenye maarifa; Na mwenye roho ya utulivu ana busara".

Wanandoa watafute ufumbuzi wa matatizo yao wao wenyewe kwanza huku kila mmoja akijitathmini na kuangalia ana mchango gani katika tatizo lililojitokeza. Wakiwashindwa ndipo watafute msaada kwa watu wengine wenye busara na hekima. Mwanandoa awe mwepesi kutambua makosa yake, kuomba msamaha na kudhamiria kujisahihisha.

Tabia ya kuweka vinyongo moyoni hushawishi visasi. Ni muhimu ikafahamika kuwa, roho ya visasi huwa haileti suluhu, bali huongeza maumivu na kuondoa uwapo wa Mungu. Wanandoa waikatae roho hii na wajenge tabia ya uwazi na ukweli ndani yao. Uwazi na ukweli huleta uponyaji wa nafsi.

Pamoja kwamba simu za mkononi ni chombo binafsi cha mawasiliano, wanandoa wanaweza kushirikishana na kuamua namna bora ya matumizi ya simu zao kadri watakavyoona inafaa.

Mara nyingi wanandoa wanaoaminiana na kuheshimiana hawawekeani mipaka ya matumizi ya simu zao. Yeyote miongoni mwao anaweza kutumia simu ya mwenzake pale inapobidi. Aidha, hujulishana nywila (password) ya simu zao, kwani kufanya hivyo ni uthibitisho kuwa, mawasiliano yanayofanyika miongoni mwao hayana shaka. Utaratibu huu unatengeneza mazingira ya wanandoa kuaminiana zaidi.

***Itaendelea Jumapili ijayo.***

***Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.***

# MAISHA

Agosti 22, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*


Ukurasa 15



## MAISHA NI NYUMBA

## Hizi ndizo mbinu za kufanya jiko lako ling'ae wakati wote

## Hivi ndivyo Lusekelo Martin Kilimba na Esta walivyoanza maisha yao ya ndoa takatifu

iliyofungwa tarehe 12/6/2021 Kanisa la Morovian Mbalizi na kufuatiwa na sherehe iliyofanyika katika ukumbi wa Tughimbe Hoteli, Mbalizi Mbeya



HARUSI

Ukurasa 12

## Vyakula hivi vinaimarisha mwili




Ukurasa 14

Ukurasa 13


# SKAFU INATOSHA KUKUNOGESHA




## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
SAI, IPO, INA, TAI, FIKA, NUKA, SANIFU, KATIZO

MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





## WATOTO

# PAKA RANGI



## CHEKA KIDOGO



SWALI

Ziwa Tanganyika linapakana na mikoa mingapi ya Tanzania?

MTOTO mmoja aliitwa na mama yake kwa ajili ya kumwogesha na kumkata kucha zake za mikononi. Baada ya kuona mama yake kashika kiwembe yule mtoto akaanza kuuliza.

Mtoto: Eti mama, hicho ni kiwembe?

Mama: Ndio mwanangu, ukimaliza kuoga nataka kukata kucha zako

Mtoto: Basi ntakuwa siliii

Mama: Safi sana mtoto mzuri huwa halii akikatwa kucha

Mtoto: Mwalimu alituambia 'mtoto akililia wembe mwache umkate'

Mama: Mwanangu huo ni usemi tu, unamaanisha msiwe ving'ang'anizi kwa mambo msiyoyaweza.

# MAISHA NDIVYO YALIVYO
## Na Flora Wingia



# Ijue siri ya ardhi na fujo za wenyeji unaowakuta maeneo unayoishi

KARIBU tena msomaji wangu katika gurudumu hili la Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo hebu nikupe siri ya ardhi na jinsi inavyogusa maisha yako ya kila siku. Ardhi tunaiona kama kitu cha kawaida sana lakini imebeba siri nzito zilizojificha.

Ardhi au udongo una siri kubwa sana kuhusu kufanikiwa au kuanguka kwa mtu katika nyanja mbalimbali kimaisha. Ardhi au udongo ni sehemu ya juu ya dunia tunayoikanyaga, tunayojenga nyumba na kuishi. Mafanikio ya mtu yanaweza kuchangiwa na aidha mahali alipozaliwa au ardhi ya mahali alipokulia, anapoishi au anapofanyia kazi. Ardhi ulipo inaweza kuchangia wewe kwenda au kutokwenda, kuinuka au kutoinuka. Yaani ardhi ina mchango mkubwa sana kwa maisha yako.

Watu wengi leo wanateseka kwa sababu ya ardhi wanayoishi. Kuna ardhi ukikaa unaishia kuwa mtu wa madeni. Zipo ndoa nzuri zimekaa nyumba za kupanga, lakini walipohamia kwenye nyumba zao walizojenga, ndoa zikaparaganyika. Ukiona dalili hizo hapo lipo tatizo.

Wapo watu wamenunua ardhi kwa ajili ya kilimo lakini wasivune kwani kila mwaka ni hasara hata kufikia kukata tamaa na kuondoka au kuiuzwa kwa watu wengine. Kumbe hawakufanya udadisi kujua historia ya waliowakaribisha kwenye ardhi ile.

Wenyeji wako ambao naweza kuwaita 'wenyeji wa nchi', ulipaswa kujua tabia zao ili ujipange kujua namna ya kuendana nao. Wenyeji ni wale waliotangulia kuwepo mahali kabla yako. Hawa watu, wengi wao ni wabaya kuliko unavyofikiria.

Watu wengi hatua zao za maisha zimeuliwa na wenyeji waliowakuta mahali fulani. Hakuna eneo lisilo na wenyeji. Popote pale mtu alipo au anatarajia kuwepo, ni lazima awakute wenyeji hata kama yeye hawafahamu. Wenyeji utawakuta nyumba uliyopanga, sehemu ya biashara, ofisini unakofanyia kazi na hata vyuoni na mshuleni.

Ni muhimu kupeleleza, kudadisi unapokusudia kukaa kwa shughuli yoyote ili ukiamua kujitosa ujiandae kwa lolote litakalotokea na ujue namna ya kujihami. Lazima uwe makini kila sehemu ulipo au unakotarajia kwenda kwani utakutana na wenyeji maeneo hayo. Kama una uhakika wa eneo fulani kwamba Mungu ameachilia baraka zako hapo, hupaswi kuogopa. Kinachotakiwa ni kujua hao utakaowakuta wana uwezo na nguvu kiasi gani, ili uwe na hekima na nguvu ya kupambana nao hatimaye uweze kuishi kwa furaha na amani.

Hawa wenyeji wanazo tabia nyingi tofauti. Hebu hapa tuone tabia tatu. Kwanza hawapendi kuzidiwa na wageni. Mtu mgeni anapotokea kuonyesha mafanikio makubwa mahali walipo, wenyeji watatumia kila njia kumwangusha. Hawataki ujenge nyumba nzuri, uwe na gari zuri wakati wao hawana. Pili, hawapendi mgeni atawale. Kuwatawala watu uliowakuta eneo ulilonunua ili kuishi, ukoo, mtaa au kazini, kunahitaji nguvu ya Mungu. Tatu, wenyeji kuwa na kitu kipya. Hata wakiona unakula vizuri, unavaa vizuri kuliko wao hawataki. Lakini watakupiga vita.

Kulingana na mtizamo wao na yale mazoea ambayo wamekuwa nayo muda mrefu, huamini kuwa kila kitu kipya kitaletwa na wao. Wapo watu wamefukuzwa kwa fitna maofisini kwa kuwa wameonekana kufanya kazi vizuri kuliko wengine. Wengine kupoteza maisha kwa njia za ushirikina, kisa wivu wa mafanikio.

Mtu mmoja akasikika akisema; "Huyu amekuja jana tu, ni mgeni halafu atutawale, hatutakubali, tutammaliza". Watu wengi wamefungwa gerezani kwa kesi za kubambikiziwa, wengine kufa vifo vilivyosababishwa na wenyeji.

Ukitaka kufahamu uwepo wa hawa wenyewe pale ulipo, fanya tu jambo, utaona vita yao. Watakupenda kabla hujawa na kitu cha kuwazidi. Lakini utakapoanza kuonyesha mafanikio kuliko wao ni lazima watakushambulia.

Mpenzi msomaji, ni muhimu utambue kwamba kila nyuma ya wenyeji zipo roho zinazowapa nguvu ili kuwashambulia wageni. Hawa wenyeji hawana dogo, hata kama utazaa mtoto mweupe kuliko wao ni tatizo. Kuwa na elimu kuwazidi ni shida.

Wiki ijayo nitaelezea aina za ardhi na siri iliyoko ndani yake. Pia nitatoa mfano wa vita niliyokumbana nayo baada ya kununua kipande cha ardhi huko Mlandizi. Je, una maoni au kisa cha maisha? Tuma ujumbe kupitia 0715268581.

# NAWAZA KWA SAUTI
## Na Salome Kitomari



# Ukusanyaji mapato kituo cha mabasi Magufuli uboreshwe

MSAFIRI au msindikizaji yeyote anayetumia kituo kikuu cha mabasi cha Magufuli kilichoko Mbezi Mwisho, Dar es salaam, anatakiwa kulipa fedha wakati wa kuingia na hupewa risiti ambayo huchanwa mara baada ya kupita.

Kwa sasa anayeingia na gari ana eneo la kuegesha na kama anamsindikiza msafiri anatakiwa kulipia kuingia kituoni na wakati wa kutoka analipia gari lake.

Naelewa kabisa bado ujenzi wa kituo hicho unaendelea na hakijakamilika kwa kiwango kilichokuwa kinatakiwa kwa mujibu wa mchoro na sasa mabasi yote lazima yaingie kituoni humo na kutoka bila abiria lengo ni kupata fedha.

Kuna mambo yanaendelea kituoni hapo ambayo yanakwamisha fedha kukusanywa na ni muhimu kuyasema ili mapato ya serikali yasipotee bure. Kuna ujanja unafanyika kwamba unapofika getini unaweza kutoa fedha na usipewe risiti na hata ukipewa haichanwi bali anapewa mwingine ambaye ataonyesha kuitaka.

Maana yake kuna uhusiano mkubwa baina ya anayekusanya na anayelinda mlangoni kwa kuwa anayekusanya fedha anachukua fedha na kutoa risiti halafu abiria akifika getini anakutana na mlinzi anayechukua karatasi na kuichana kisha kuweka kwenye chombo cha takataka.

Kama msafiri ana watu wanne ameambatana nao ataambiwa alipie wawili Sh. 300 na wengine asiwalipie lakini asipewe risiti yoyote. Maana yake hiyo fedha inakwenda kwenye mikono mingine.

Pia wakati mwingine risiti zinapopokelewa na mlinzi hazichamwi bali zinarudi tena kwa kutoa risiti ili apewe abiria mwingine jambo ambalo ni dhahiri kuwa fedha nyingi sana inapotea kituoni humo.

Abiria anapopewa risiti hiyo hapewi nafasi ya kuangalia karatasi aliyopewa inakuwa namna fulani ya kumharakisha ili akabidhi karatasi kwa mlinzi ambaye huchana au asichane. Kama amepewa 10 basi huchana tano na tano kubaki nazo ambazo hurudi mikononi kwa mkusanyaji.

Kwa upande wa magari unapotoka unalipa Sh. 500 na unapewa risiti iliyoandikwa kiwango sahihi na unaruhusiwa kuondoka nayo.

Kwa ujumla utaratibu huu unapoteza mamilioni ya fedha kwa kuwa kuna udanganyifu mkubwa kituoni humo na inapeleka salamu kwa mamlaka kuwa wanapaswa kuweka mfumo mziri wa ukusanyaji fedha.

Ipo mifumo mbalimbali inatumiwa duniani ikiwamo wa kuachana na fedha taslimu na kuwa na kadi maaalum ambayo mtu huilipia kabla, kwamba anapofika kituoni anachanja kwenye mashine inamruhusu kupita.

Wengine huweka mashine ambayo mtu huingiza fedha inayotakiwa na kupata risiti, mathalani kwenye mabasi hakuna kondakta bali unalipa nauli na kupewa risiti kwa mashine.

Kinachofanyika ni ukaguzi wa mara kwa mara na unapokutwa ndani ya basi huna risiti ya malipo ya nauli utawajibika kwa kulipa faini kubwa sana, jambo ambalo linawalazimisha wengi kutii na kulipa nauli bila kushinikizwa.

Ni lazima kituoni humu kuwekwa utaratibu sahihi wa kukusanya fedha vinginevyo ni mchezo mchafu unaoendelea ambao unapoteza mamilioni ya fedha na huku wengine wakitozwa mara mbili.

Kwa mfano, mwenye gari anatozwa mara mbili kwamba ameingia na gari analipia gari kuingia naye anajilipia nauli kuingia ndani jumla Sh.800, jambo ambalo siyo sawa pia.

Bila kufuatilia kwa karibu serikali inapoteza fedha nyingi sana kwenye kile kituo na bila maboresho ni wazi kuwa kinachokusanywa ni kidogo kuliko kinachopatikana jambo ambalo si sahihi.

Kama nchi tumewekeza fedha nyingi eneo hilo ambazo ni mkopo ni muhimu sana zinafuatiliwa na kurudi kwa kuwa mirija inayovuja ni mingi sana kwenye kituo cha Magufuli na huenda kinachokusanywa ni robo ya kinachotakiwa kukusanywa.

**Mungu ibariki Tanzania**



# Hivi ndivyo Lusekelo Martin Kilimba na Esta walivyoanza maisha yao ya ndoa takatifu

iliyofungwa tarehe 12/6/2021 Kanisa la Morovian Mbalizi na kufuatiwa na sherehe iliyofanyika katika ukumbi wa Tughimbe Hoteli, Mbalizi Mbeya






Tunachapisha picha za harusi bure wasiliana kwa namba 0717336368, au barua pepe: moshilusonzo@gmail.com”

# MITINDO

# SKAFU INATOSHA KUKUNOGESHA







**Na Mary Geofrey**

UNAWEZA kuongeza uzuri wako kwa kuongeza nakshi ya kichwani kwa kuvaa skafu au wengine wanaita Bandana.

Ubunifu wa kubadili skafu ya kichwani na kunogesha mwonekano wako inasaidia kukupa umaridadi katika vazi ulilopigilia.

Wanawake wamekuwa wakiumiza kichwa kuhusu watoke vipi kwenye suala la mavazi, viatu na nywele.

Mara nyingi nywele wanazosuka zinaamua uvae vazi gani ili udamshi zaidi.

Kwa wale ambao wamesuka nywele ya muda mrefu, skafu ya kichwani itakufanya uonekane mpya kila siku.

Unaweza kufunga skafu yako kulingana na rangi ya kiatu au vazi ulilopigilia na ukabadili kila siku.

Skafu ya kichwani unaweza kuifunga mwenye nywele fupi au ndefu inategemea tu na mpangilio wako.

Mara nyingi hufungwa kwa kitambaa kilichokunjwa kwa mfumo wa pande nne, ikiacha pembe mbili ndefu (kwa vitambaa vya pande nne), unakikunja mara nne zaidi.


Baada ya kuwa usawa unaotaka, pembe mbili zitakusaidia kutengeneza tai pale utakapofunga skafu yako.

Aidha, kuna vitambaa ambavyo tayari vipo katika mfumo wa skafu hivyo kazi yako ni kufunga tu.

Skafu yako unaweza kufunga kama ambavyo inaonekana kwenye picha hizi hapa.

# UREMBO:
## MACHO MEUPE YANAYOITA

# Urembo usiofahamika, wenye mvuto wa kipekee



ENEO la ndani la jicho ambalo lina rangi nyeupe kitaalamu huitwa sclera, weupe wa eneo hili ni dalili nzuri kwamba mtu husika ana afya njema.

Katika suala la urembo kuwa na macho yenye rangi ya njano au nyekundu sio dalili nzuri.

Watu maarufu hasa wa nje ya nchi huonekana na macho meupe sana, mwonekano huo si jambo la bahati, bali kuna utaratibu wanaoufuata.

**Dawa ya kusafisha macho.**

Kuna dawa ya matone ya macho kama 'Clear Eyes na 'Eye Drops' ambayo unaweka machoni angalau kutwa mara nne

Matone haya huondoa mwasho na ukavu wa macho na kuyaacha yakiwa na unyevunyevu.

Kula matunda na mbogamboga

Vyakula hivi vina vitamini muhimu kwa ajili ya macho, kama A, C na E ambazo kimsingi ndio muhimu sana kwa ajili afya ya macho.

vyakula hivi pia huisaidia kuondoa sumu mwilini.

**Pata usingizi**

Binadamu anatakiwa alale angalau masaa saba mpaka nane kwa siku, ukichunguza mtu aliyekosa usingizi hata siku moja huwa na macho mekundu kwa sababu ya uchovu.

**Kunywa maji**

Unywaji wa maji angalau glasi nane mpaka 10 kwa siku unasaidia kusafisha mwili wote na kuondoa sumu pia kuondoa uvimbe kwenye macho.

**Vaa miwani ya jua**

Mara nyingi huwa tunaona watu maarufu wanavaa miwani nyeusi, hawavai kwa urembo bali kwa kufanya macho kuwa meupe.

Miwani nyeusi inakinga macho dhidi ya miale ya jua iwapo ikikupata kwa muda mrefu.

**Mtandao.**

# MAPISHI
## Na Mary Geofrey

# VYAKULA HIVI VINAIMARISHA MWILI



MLO kamili ni ule unaozingatia makundi yote ya vyakula.

Ili kupata mlo kamili unapaswa kuzingatia matunda, mboga za majani na maji.

Leo tunakumbushana vyakula ambavyo husaidia kuulinda mwili dhidi ya maradhi mbalimbali pamoja na kuufanya mwili kuwa na nguvu.

Kuna aina nyingi za vitamini zinazopatikana kwenye mboga za majani, matunda, dagaa au samaki na vyakula vinavyotokana na wanyama kama maziwa mayai, aina zote za nyama na nafaka.

Makundi ya vyakula vya vitamini ni kama A, B, C, D, E, K

**VITAMINI A**

Hii husaidia ukuaji wa mwili na akili, kuimarisha seli za ngozi kuimarisha Kinga ya mwili dhidi ya maradhi na husaidia macho kuona vizuri.

Vitamini A hupatikana kwenye vyakula kama maini, figo, samaki mboga za majani za kijani na viazi vitamu vya rangi, machungwa, karoti, nyanya, matunda hasa yenye rangi ya njano au nyekundu.

Upungufu wa vitamini A husababisha kutoona kwenye mwanga hafifu na maradhi ya kuambukizwa mara kwa mara kwenye mfumo wa hewa.

# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

## HIZI NDIZO MBINU ZA KUFANYA JIKO LAKO LING'AE WAKATI WOTE



UTUNZAJI wa nyumba ni pamoja na upangiliaji mzuri wa jiko na namna ya kuliweka katika mazingira safi ya kuvutia.

Pia utunzaji mbaya wa jiko huchangia kuharibu mvuto wa nyumba kwa sababu kitu kimojawapo katika nyumba iliyo bora kisipowekwa katika mazingira bora, kinaweza kuvuruga au kuharibu kabisa mvuto wake ambao unakuwa umekusudiwa katika nyumba husika.

Kanuni muhimu ya mvuto na unadhifu katika kila kitu kilichomo katika nyumba yako ni usafi na mpangilio wake, kwamba kisiwe kikwazo cha kuharibu mwonekano wa nyumba.

Na nyumba nyingi katika kipindi hiki cha sayansi na teknolojia, hata majiko ya kupikia yanatengenezwa moja kwa moja wakati nyumba inajengwa. Lakini hata kwa yale yasiyotengenezwa wakati wa ujenzi wa nyumba husika, yanatakiwa yawekwe katika mpangilio bora bila kuathiri mvuto wake.

Miongoni mwa siri za kufanya jiko liwe safi wakati wote ni pamoja na kuhakikisha unapokuwa unaandaa chakula, jenga utamaduni wa kuepuka kurundika vyombo vichafu. Jitahidi vile vinavyochafuka unaviosha. Epuka michuzi ya chakula unachopika isirukie ukutani na hata kama kwa bahati mbaya. Hakikisha unasafisha kabla haijakauka.

Jiwekee utaratibu kwamba unapokuwa unapika chakula. Tumia ule muda ambao unasubiri kiive kuosha vyombo vyako unavyochafua na kuweka kila kitu sawa jikoni kwako.

Punguza mrundikano wa vyombo kwenye meza ya jikoni au sinki ili kuleta wepesi wa kufanya usafi kwa sababu unapokuwa na vitu vingi ndivyo unavyoharibu mwonekano wa jiko lako na hata kujipa kazi kubwa unaposafisha baadaye na wakati mwingine unapotembelewa na wageni gafla ni rahisi ukashindwa kuvitelekeza.

Hakikisha vyombo vingine kama visagio na vibao vya kukatia, vya kusukumia chapati na vya kusagia viungo vinahifadhiwa kabatini hadi wakati wa matumizi yake unapofika.

Usafi wa jikoni ni sehemu ya kustawisha nyumba, unatakiwa uwe ni wa mara zote na wa kudumu kwa sababu haipendezi kusafisha sebuleni halafu ukaacha jikoni kuchafu, huo utakuwa ni utunzaji mbovu wa nyumba.

Ni vyema kuhakikisha pia kuwa kila chombo ama kifaa cha jikoni kina mahali pake, sio leo kipo kabatini, kesho mezani mara chini ya meza.

Usafi pia wa sakafu la jikoni unapaswa kuzingatiwa na ni vema kuhakikisha kila siku kabla ya kulala vyombo vyote vinakuwa safi, vinakaushwa na kupangwa mahali pake ili unapoamka kesho yake unafanya usafi wa kawaida.



# MPANGILIO

## DONDOO MUHIMU ZA KUCHAGUA MAPAZIA YA SHANGA

MAPAZIA ya shanga yanajulikana kama Filament, ni mazuri katika kupamba madirisha ya nyumba yako. Hizi ni baadhi ya dondoo ambazo zitakusaidia kupata mapazia mazuri.


1: Zingatia wepesi wa kamba ya pazia ili kufanya kutokuwa nzito inapowekwa dirishani.

2 Tazama rangi ya pasia kama inaweza kukupa mwonekano mzuri wa macho, hairuhusu hewa kupita au kuchafuka haraka.

3: Hakikisha shanga zilizowekwa katika kamba za mapazia kama ni halisi na zenye ubora unaokubalika.

4: Mapazia bora ya aina hii yanatokea Urusi, hakikisha kama mapazia hayo kuna alama zozote zinazoonyesha sehemu yalipozalishwa.




KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
MZIMU HAUSINZII WALA HAULALI...
'ghosh!!!'
WAPIGAJI
WEWE NI SEKRETARI, KWANINI UMEKUJA KAZINI NA POMBE?
KWANI MWENZANGU IMEKATA?
NENDA KAMUANGALIE JAMBAZI ANA SILAHA GANI?
NIMESHAIONA BADO WEWE TU KUIONA
UNAVYOBWABWAJA BILA KUVAA BARAKOA KAMA UNAO UJUE UMETUMALIZA!
SIO BARAKOA TU MUULIZE ANAJUA KAMA KUNA ZOEZI LA KUCHANJA?
NYAMAZA WEWE! KORONA IPENYE WAPI WAKATI MUDA WOTE NIMELEWA VIKALI
WEWE USHAJIKATIA TAMAA UNAJUA MAINI YAKO YAMEOZA
HUYO MLEVI ANACHOJUA 'KUCHANJA MBUGA' SIO VINGINEVYO!
KATUKATA STIMU!
DAR
'MBABE' ANYOLEWA 'KIDUKU' NDINGA YATUA MORO
AFYA KWA FAIDA YAKO LAKINI MPAKA UKEMEWE NDIO UVAE BARAKOA!
ULIYOVAA UMEINUNUA WAPI?
USIPOCHANJA ITAFIKA WAKATI UTAJIONA KAMA 'KUNGURU' KWENYE KUNDI LA NJIWA
MWE!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UPATAPO FAHAMU UJUE UMEPOTEA



Umati wa watu wakiwa nje ya uzio wa uwanja wa ndege mjini Kabuli, nchini Afghanistan, wakisubiri kuingia ndani kwa ajili ya kusafirishwa kwa ndege kwenda mataifa mengine. **(PICHA: BBC)**

# Maelfu watanda uwanja wa ndege kuomba kusafirishwa ukimbizini

**KABUL, Afghanistan**

TAHARUKI imetanda nchini kote Afghanistani, huku maelfu ya watu wakiendelea kukusanyika eneo la uwanja wa ndege wa Kabul, kwa ajili ya kuomba msaada wa kuhamishwa nje ya nchi.

Wanajeshi wa Uingereza wakisaidiwa na wale wa nchi hiyo, kwa siku tatu wanakabiliana na umati wa watu ambao wanataka kuondoka nchini humo baada ya kundi la Taliban kutwaa madaraka.

Baadhi ya watu waliojazana uwanjani hapo, walikuwa na hati zao za kusafiria za Uingereza, wakitumaini kuruhusiwa kupita, lakini kundi la walinzi waliobeba mipira walijaribu kuwarudisha nyuma.

Hata hivyo, umati huo hawajaambiwa chochote kama watahamishwa, lakini walionekana kutokata tamaa ya kuondoka katika nchi hiyo.

Hata hivyo, baadhi ya watu hao walikuwa wamepokea barua pepe kutoka kwa ubalozi wa Uingereza, wakiambiwa wafike hapo na kusubiri kushughulikiwa kupata ndege ya kuondoka nayo.

Helmand Khan, dereva wa Uber kutoka magharibi mwa London, ambaye alikuwa amewasili na watoto wake wadogo miezi michache iliyopita kwa ajili ya kutembelea jamaa, alisema kwa siku tatu hajafanikiwa kuingia ndani ya uwanja huo kwa ajili ya kuanza safari.

"Kwa siku tatu najaribu kuingia ndani, lakini sijafanikiwa," alisema akiwa amekata tamaa.

Khalid, ambaye alikuwa mkalimani wa jeshi la Uingereza, alisema anaogopa mkewe na mtoto wao wanaweza kupata matatizo kutokana na vurugu zinazotokea kwenye eneo la uwanja.

"Nimekuwa hapa tangu asubuhi, Wataliban walinipiga mgongoni nilipokuwa njiani," alisema Khalid.

Hata hivyo, huwezi kutembea kuelekea mlango mkuu wa kuingia uwanjani kutokana na maelfu ya watu kujitokeza, idadi ambayo haikutarajiwa kujitokeza kwa ajili ya kuhamishwa.

Wanajeshi wa Uingereza wakati mwingine walifyatua risasi hewani kudhibiti umati.

Njia pekee ya kuingia ndani ni kwa kushinikiza kupenya katikati ya umati wa watu, na kupunga hati zao, wakitumaini wataruhusiwa kupita.

Hali kama hiyo ilionekana pia katika milango ya uwanja wa ndege iliyo na wanajeshi wa Marekani.

Upande wa mbele wa mlango mkuu wa uwanja wa ndege, kuna wanamgambo wa Taliban, wamekuwa wakifyatua risasi hewani mara kwa mara ili kuzuia umati wa watu ambao wanajaribu kuingia ndani.

"Mimi hushambuliwa kila wakati na maswali na Waafghanistan ambao wanajaribu kuingia kwenye kiwanja kinachodhibitiwa na Uingereza na ambao wamepoteza kabisa matumaini," alisema msichana mmoja ambaye alikuwa mchezaji wa mpira wa magongo.

Alisema hajapata mawasiliano yoyote na ubalozi wa Uingereza, lakini anahofia maisha yake.

Taliban walisisitiza wale wote wanaohusishwa na serikali wamepewa msamaha.

Kundi hilo linasema linakusudia kuanzisha serikali ya umoja, lakini wengi wana wasiwasi mkubwa kuhusu ya siku zijazo.

Mahali pengine katika jiji hilo, mambo yametulia na kuonekana kama ulimwengu wa tofauti.

Maduka na migahawa ilifunguliwa, ingawa kwenye soko la matunda na mboga mboga bado kuna watu wachache.

Wakati huo huo, wanamgambo wa Taliban wametanda kila mahali, wakifanya doria katika magari yaliyokamatwa kutoka kwa vikosi vya usalama vya Afghanistan.

Walisema wanadumisha amani ili kuzuia uporaji na machafuko.

**BBC**

## Cuba yaidhinisha chanjo tatu corona

**HAVANA, Cuba**

SERIKALI ya Cuba imeidhinisha chanjo mbili mpya dhidi ya virusi vya corona, zinazoweza kutumiwa katika kipindi cha dharura.

Kulingana na taasisi ya kudhibiti madawa kisiwani humo (SECMED), ilisema ilitoa idhini hiyo kufuatia mchakato mkali wa majaribio ya chanjo hizo za Soberana 02 na Soberana Plus. Tangu mwezi uliopita.

Cuba ilikuwa taifa la kwanza la Amerika Kusini, kutengeneza chanjo ya kinga ya virusi vya corona iliyoitwa Abdala.

Mamlaka ya afya ya nchi hiyo, ilisema chanjo za Soberana zinatoa kinga ya asilimia 91.2 dhidi ya virusi vya corona.

Chanjo hizo zinajumuisha dozi mbili za Soberana 02 ikifuatiwa na dozi moja ya tatu ya Soberana Plu.

Chanjo ya Abdala pia inahitaji dozi tatu.

Kufikia Agosti 18, nchi hiyo yenye watu milioni 11.2 ilikuwa tayari imeshatoa dozi za chanjo milioni 12.3.

**DW**

## Hukumu ya Rusesabagina yaahirishwa

**KIGALI, Rwanda**

HUKUMU ya kesi inayomkabili Paul Rusesabagina, ambaye alishiriki katika filamu inayoelezea mauaji ya halaiki ya Rwanda ya mwaka 1994, inayoitwa Hotel Rwanda, umesogezwa mbele.

Rusesabagina anayejulikana kama shujaa kwa kuokoa maisha ya watu elfu moja wakati wa mauaji hayo, aliondoka nchini Rwanda kabla ya kuwa mpinzani na mkosoaji mkuu wa Rais Paul Kagame.

Mwaka mmoja uliopita, alikamatwa na kutekwa nyara kulingana na familia yake, na kurudishwa Rwanda ambako tangu wakati huo anakabiliwa na mashtaka ya ugaidi.

Hukumu iliyokuwa ikisubiriwa kwa muda mrefu ambayo ilipangwa kutolewa Alhamisi, Agosti 19, mwaka huu, imeahirishwa hadi Septemba 20.

Kesi hiyo iliahirishwa kwa kipindi cha mwezi mmoja kwa sababu ya ukubwa wake, mahakama ya Rwanda ilisema.

Hukumu hiyo itacheleweshwa kwa mwezi mmoja kabla ya kujua hatima ya Rusesabagina, ambaye anakabiliwa na kifungo cha maisha na washtakiwa wenzake 20.

**RFA**

SAFU

# Wajibu wa wanasiasa kwa wananchi



Na Magabilo Masambu

MWANAFALSAFA wa zamani wa Ugiriki, Aristotle aliwahi kusema: "Every human being is a political animal" akiwa na maana kwamba kila mwanadamu ni mwanasiasa! Anasema siasa ni hali ya kufikia makubaliano kwa njia ya ushawishi na kujenga uhusiano. Yaani kama umewahi kufanya jambo lolote ukafikia makubaliano na mwingine basi wewe ni mwanasiasa.

Anajaribu kuwafananisha wanadamu na ndege wanyama kwamba tabia ya kuruka na kupaza sauti mwituni huzaliwa nayo ni asili hata siasa ni hivyo. Jiulize katika maisha yako yote hujawahi kumshawishi yeyote mkakubaliana? Kama umewahi na ukafanikiwa wewe ni mwanasiasa nguli.

Natambua wako watu wanasema kila siku kwamba wao si wanasiasa wakidhani kwamba siasa lazima pengine uwe diwani, mbunge au rais wa nchi jambo ambalo si kweli.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 8(a), (b), (c) na (d) inasema "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii na kwa hiyo - (a) wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii, (b) lengo kuu la serikali litakuwa ustawi wa wananchi, (c) serikali itawajibika kwa wananchi, (d) wananchi watashiriki katika shughuli za serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

Kwa mujibu wa ibara hii ya katiba, wananchi ndiyo wenye nchi, uamuzi wowote utakaofanywa na wanasiasa lazima uzingatie misingi ya demokrasia. Bahati mbaya tulio nayo Afrika ni kudhani kwamba demokrasia ni kuwa na vyama vingi vya siasa pekee. Lakini uamuzi wowote unaohusu maisha ya watu lazima uwe umepata nguvu ya ushawishi badala ya ushawishi wa nguvu. Hata ushiriki huo uliotajwa na katiba kipengele (d) lazima uwe umejengwa katika misingi hiyo.

Wajibu mkubwa wa wanasiasa si kuwaletea wananchi maendeleo. Katika hili wanasiasa wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana kuwafanya watu waamini kwamba maisha yao yatajengwa na wao na kwamba bila wao maendeleo hakuna, jambo ambalo si kweli kwa sababu hakuna mwanansiasa hata mmoja anayetumia fedha yake mfukoni kuleta maendeleo. Fedha hizo zitakuwa zimetokana na rasilimali zetu za nchi, kodi au mikopo ambayo pia walipaji ni wananchi au misaada kutoka nje.

Kipengele (b) ibara ya 8 kinasema lengo kuu la serikali litakuwa ustawi wa wananchi, ustawi wa jamii si katika eneo moja tu la maendeleo ya vitu kwa maana ya mabarabara mazuri, mwonekano mzuri wa miji nakadhalika.

Ustawi huo ni pamoja na uhuru wao, kuongozwa kwa mujibu wa katiba, kuwa na uhuru wa kusema hili sawa, hili hapana na wakisema hili hapana katiba ilinde uhuru huwo na kazi ya wanasiasa iwe ni kutumia hoja nzuri za kuwashawishi wakubali kwa hiari yao baada ya kuelewa vema juu ya jambo lenyewe.

Kwa maana nyingine, wajibu wa wanasiasa ni kuwakilisha mawazo na maoni ya wananchi pamoja na kuwaunganisha. Ndiyo maana tunavyo vyombo vya uwakilishi kama bunge na kwa sababu wananchi ndio waajiri kwa mujibu wa kifungu kidogo(a) cha ibara ya 8 maoni na malalamiko yao ni muhimu kusikilizwa ama kuyafuta malalamiko au kuwashawishi waone umuhimu wa kutekeleza jambo fulani wanaloona haliko sawa.

Nakubali kwamba si mambo yote yanayopaswa kutekelezwa na wanasiasa yawe ni ya wananchi, yatoke kwa wanasiasa pia maana wao nao ni sehemu ya wananchi. Kazi kubwa watakayokuwa nayo si kutumia nguvu kuyalazimisha mawazo yao, bali kujenga hoja juu ya mambo hayo.

Mtu yeyote atakayeshindwa kujenga hoja ya ushawishi badala yake akatumia nguvu kulazimisha jambo fulani lifanyike, lazima ajihesabu kwamba siasa imemshinda achukuwe jembe akalime akiendelea atasababisha matatizo makubwa.

Katika eneo la maendeleo lazima tubadili fikra za kuamini kwamba sisi wananchi tunatakiwa kuletewa maendeleo na wanasiasa, bali wanasiasa wanapaswa kuweka mazingira wezeshi na usimamizi mzuri wa rasilimali zetu ili wananchi wajiletee maendeleo wenyewe.

Kama tutakuwa na wanasiasa wanaoshindwa kusimamia rasilimali zetu ndani ya nchi katiba imetupatia nafasi ya kuwaondoa katika nafasi zao kupitia sanduku la kura kwasababu watakuwa wameshindwa kutenda wajibu wao kama wanasiasa.

Siasa ni nyepesi sana kama zitatumika akili za kutosha badala ya nguvu ambazo zinaweza kufanikisha jambo kwa muda mfupi na kuleta madhara makubwa. Tanzania kwa nchi za Afrika, kutokana na misingi tuliyokuwa nayo huko nyuma hasa umoja, amani na upendo, hatukuwa na nchi ya kufananishwa nayo.

Wengi walikuwa wanafunzi wetu. Sasa turudi kwenye misingi yetu ya utaifa inayojumuisha utamaduni, historia pamoja na mila zetu lakini muhimu zaidi kuenzi mambo mazuri ya wazee na vongozi wetu ambao baadhi wametangulia mbele ya haki.

***0689157789***
***magabilomjalifu@gmail.com***
***ARUSHA-TANZANIA***

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Sam Mangwana humpotezi Manzese



Na Adam Fungamwango

KWENYE miaka ya 1960 hadi mwishoni mwa miaka ya 1990, mashabiki wengi wa muziki wa dansi walikuwa hawajui habari mbalimbali za nyimbo zilizokuwa zikiimbwa.

Watu walichofaidi ni mirindimo ya muziki na sauti hasa kwa nyimbo za Kikongo ambazo wabongo wengi hawakuelewa kinaimbwa nini. Na wengine walitafsiri kivyaonyao maneno yu lugha ya Kilingala, wakayawekea maneno ya Kiswahili. Nyimbo za kiswahili ndizo zilizokuwa zikieleweka kimeimbwa nini, achilia mbali midundo na mirindimo ya muziki wenyewe.

Pamoja na yote hayo, labda kutokana na uchache wa vyombo vya habari, au kutokuwepo kwa utandawazi, wengi hawakuelewa sababu za kutungwa nyimbo zile na nani alitungiwa, nini kilitokea na kwenye mazingira gani.

Kwenye safu hii, tutakuwa tukiwaletea pia sababu ya baadhi ya nyimbo kutungwa, nani alitungiwa na ilikuwaje. Leo tutamzungumzia mwanamuziki raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Sam Mangwana.

Ni mwanamuziki maarufu sana tangu mwanzoni mwa miaka ya 1970 na hadi leo yuko hai na anaendelea na shughuli za muziki. Amezipigia bendi kubwa nchini Congo DR za TP OK Jazz chini ya Hayati Luambo Luanzo Makiadi Franco, na Afrisa International, chini ya hayati Tabu Ley Rochereau.

Huyu jamaa ni Mkongomani aliyezaliwa Leopoldville ambayo kwa sasa ndiyo Kinshasa, mji mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo. Wazazi wake hawakuwa Wakongomani. Baba yake alikuwa Mzimbabwe na mama yake alikuwa raia wa Angola.

Ni mmoja wa wanamuziki wachache wanaojua lugha nyingi mno. Akiimba Kiswahili unaweza ukadhani amezaliwa Dar.

Ambalo mashabiki wengi wa Bongo hawajui ni kwamba huyu jamaa aliishi sana Tanzania, hasa jijini Dar es Salaam mwanzoni kabisa mwa miaka ya 1980. Pia si wengi wanaojua kuwa alishawahi kupigia bendi za Maquiz du Zaire na Vijana Jazz Band.

Nyimbo za 'Mary Maria', 'Tambiko la Pambamoto', na 'Bujumbura' ambazo zilitungwa na hayati Hemed Maneti, kwa kiasi kikubwa zilichangiwa na Mangwana kwenye utengenezaji wake hadi zikakaa sawa. Ndiyo maana ukichunguza nyimbo hizo, uimbaji wake na upigaji ni tofauti na nyimbo za Vijana Jazz zilizopita kabla ya albamu hiyo.

Tatizo la Mangwana ni mwanamuziki asiyetulia. Huwa hakai bendi moja. Alikaa muda mfupi kwenye bendi zote mbili kama mwanamuziki mwalikwa na akaondoka zake kwenda nchini Kenya, akakaa kidogo, akaenda zake Ulaya na kwa sasa anafanya shughuli zake Ufaransa na Ubelgiji.

Akiwa nchini alikuwa anaishi maeneo ya Manzese Midizini kwa rafiki yake mmoja aitwaye Kamanga. Kila alipokuwa akija nchini alifikia hapo hadi anapoondoka. Hata akirudi leo, Mangwana humpotezi mitaa ya Manzese, anaijua vilivyo. Labda tu anaweza kushangaa kwa jinsi ilivyojengeka tofauti na alivyoondoka.

Mangwana alikuwa na marafiki wakubwa wawili nchini ambao alikuwa kila kifika wanamuwezesha kuishi hapa. Mbali na Kamanga, pia rafiki yake mwingine alikuwa Anania Sangula.

Ikumbukwe Anania aliwahi kuwa mcheza soka kwenye klabu ya Simba miaka ya 1970, kabla ya kuwa mfanyakazi kwenye kiwanda cha bia wakati huo. Kutokana na urafiki wao mkubwa na ukarimu wa hali ya juu waliokuwa wakimfanyia kila alipokuwa akija mchini, aliwatungia nyimbo mwenye miaka ya hiyo ya 1980.

Wimbo wa kwanza ni 'Kabibi'. Kwenye baadhi ya mashairi ya wimbo huo Mangawana anaimba:

"Mara ya kwanza tulipoonana alinisalimia. Aliambia ananitambua kutokana na mapicha yangu. Mwanamke mzuri kama malaika, anavyotembea ni kama nguva ndani ya bahari. Tafadhali nielezee kwenu wapi. Akasema anatoka Afrika ya Mashariki, nyumbani kwao Tanga. Usiumize Kabibi. Anania wangu yuko Dar. Sikia tabu niliyopata. Kamanga wangu Manzese."

Ni maneno ambayo Mangwana aliimba kuwataja wafadhili wake Watanzania, Kamanga na Anania.

Ukiacha wimbo wake huo binafsi aliomuimbia msichana mrembo Kabibi aliyekutana naye Tanzania, miezi michache kabla ya kifo cha Franco, Mangwana alirejea kwa mwanamuziki huyo ambaye ni kama baba yake na kutoa naye albamu moja iitwayo 'Toujours'.

Wimbo uliobeba albamu hiyo wanaimba wote Franco na Mangwana. Lakini kuna kipande ambacho Franco anaimba ni kama alipewa na Mangwana ili awataje 'washkaji' zake wa Bongo, tena kwa lugha ya Kiswahili. Wimbo huo kwa Tanzania ulikuwa maarufu kwa jina la 'Muongo na Mulozi ni Watu wa Kuchoma'.

Franco anaimba "Rafiki yake Anania wewe Mangwana. Usiwafuate endelea jamni ee, ukipata tabu omba kwa Mungu, ala Mungu mpaka yeye milele na milele." Mwishoni kabisa mwa wimbo, Mangwana anamalizia na maneno ya Anania Dar es Salaam, ye.

Huyu ndiye Sam Mangwana, mwanamuziki mkubwa wa Kikongo anayejua vizuri lugha ya Kiswahili na mitaa ya Manzese kama Mbongo tu.

***Kwa mawasiliano piga 0716 350534***

# HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana?
Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa.
Donald. Kijana msomi aliyetoka nchini Marekani, anarejea nchini Tanzania. Akakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake. Lakini pia anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

# Sumu ya mapenzi-20

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Okay, sasa afande nini kinafuatia?" Koplo Peter aliuliza.

"Ni hivi kesho pumzika. Kesho kutwa anatakiwa mpenzi wa marehemu Tausi aletwe hapa."

"Akamatwe?"

"Hapana. Awamu ya kwanza itaanza kwa mahojiano. Tukiona inaelekea kama yeye anahusika, basi hatoondoka, lakini tunaweza pia kupata kitu kingine ambacho tunaweza kuona kwanza tumuachie ili tumfuatilie kuona nini kinatendeka. Hizi kesi mara nyingi zinakuwa na mambo mengi sana."

"Sawa afande." Alijibu afande Peter. Akasimama na kupiga saluti, akatoka nje ya ofisi ya mkuu wake.

************************

"Naomba jina lako kamili, tafadhali."

"Donald Peterson."

"Unafanya kazi wapi?"

Swali hili lilimshangaza Donald kwani ni polisi hao hao walikuja kumwita kwenye ofisi ambayo wanaijua, lakini bado wanamuuliza maswali.

"PIG"

"Umeajiriwa?"

"Kampuni ya baba yangu mzazi."

"Sawa, nakuuliza umeajiriwa au na wewe una shea kwenye kampuni ya mzee?"

"Na mimi nina hisa, lakini kwa sasa mzee amejiondoa, amekuwa kama msimamizi tu. Mimi ndiyo Ofisa Mtendaji Mkuu."

Donald alijibu maswali hayo akiwa amechukia kidogo, kwani anaona kabisa aliloitiwa hapo silo hilo.

Alijua kabisa anaitiwa kutokana na kifo cha mpenzi wake Tausi. Na walichokuwa akitaka kuoanisha maswali yake na waliowauliza watu wengine.

Pamoja na kujua ukweli kuwa wazazi wake pamoja na aliyetaka kuwa mpenzi wake, Doroth wamehusika na kifo cha Tausi, lakini hakutaka kujibu kirahisi au kueleza ukweli wote kwa polisi.

Alichokuwa akihofia ni kwamba akieleza kila kitu, huenda na yeye akawa matatani. Hata kama hatoweza kwenda mahakamani kwa kesi ya mauaji, lakini anaweza kupata adhabu ya kuhusika kwa njia moja ama nyingine.

Kuonekana kujua moja kwa moja tukio hilo mbele ya polisi kulimtisha na kuona atahesabika na yeye yumo kwenye mkakati huo.

"Unamfahamu msichana mmoja anaitwa Tausi?"

"Namfahamu."

"Ni nani?" Yalikuwa ni maswali




kutoka kwenye kinywa cha Koplo Peter, akiwa ameyapangilia kiufundi na kimkakati zaidi.

"Alikua mpenzi wangu."

"Kwa sasa siyo mpenzi wako?"

"Ndiyo."

"Kwa sababu gani?"

"Amefariki dunia."

"Amefariki katika mazingira gani? Koplo Peter alizidi kumyanyasa Donald kwa maswali mfululizo, huku akiwa ameweka chombo cha kunasa sauti mezani, pia akiwa na kijitabu kidogo akiandika.

"Aliuawa maeneo ya Sinza na mwili wake kukutwa kwenye mtaro pembeni mwa barabara ya Shekilango."

"Bwana Donald, unadhani mpenzi wako aliuawa na nani?"

Donald alionekana kama anafikiri kidogo, halafu akajibu kiuchovu "Kusema kweli hata sijui mpaka sasa."

"Ulimpenda sana Tausi?"

"Hilo siyo la kuuliza afande, yule ni mpenzi wangu, na nilitaka siku moja tufunge ndoa."

"Mpenzi wako alikwenda Sinza kufanya nini?"

"Hata mimi sijui?"

"Hakukuaga kuwa anakwenda kwenye sherehe fulani na shoga zake?"

Swali hili lilimshtua Donald na wakati mwingine lilimfanya kama kutaka kucheka.

Ni kwa sababu anajua, hadaa yote iliyofanyika ya yeye kupotezewa simu, na marehemu Tausi kutumiwa ujumbe aende Sinza baadaye kuuawa.

"Hakuniaga."

"Ni muda gani ulipita hadi kupigiwa simu kuwa mpenzi wako ameuawa?"

"Siku tatu baadaye, tena niliambiwa kuwa haonekani. Baadaye nilipokwenda kwao, ndiyo nikaambiwa mwili wake umeokotwa."

"Kwa siku zote tatu, kwa nini hukumtafuta kama kweli ni mpenzi wako? Au mlikuwa mmegombana?"

"Hapana. Nilikuwa namtafuta kwenye simu lakini hapatikani."

"Mbona kuna taarifa kuwa wewe mwenyewe ulikuwa umepoteza simu yako?"

Hapo ndipo Donald alipoanza kulisifu Jeshi la Polisi kwa kujua kuwa wapo hatua tatu mbele kujua nini kilitokea.

"Ni nani aliyewaambia kuwa na mimi nilipoteza simu?" Alijiuliza mwenyewe. Alikuwa hana habari kwamba rafiki yake Sadiki ameshahojiwa na polisi. Na ni yeye mwenyewe ndiye aliyemwambia kuwa alipoteza simu siku ile alipopigiwa na kutaarifiwa kupotea kwa Tausi.

"Hukupoteza simu?"

"Ndiyo?"

"Ulipataje taarifa za kupotea kwa mpenzi wako?"

"Nilipigiwa simu na rafiki yangu sadiki."

"Alitumia namba zile zile za siku zote?"

"Ndiyo."

Baada ya kuandika maelezo kadhaa, Koplo Peter alimruhusu Donald kuondoka, lakini kwa masharti maalum ya kutosafiri nje ya Dar es Salaam, huku akikabidhisha baadhi ya nyaraka ili kuzuia kutoroka.

"Hatutaki kukuweka ndani, lakini tutachukua baadhi ya nyaraka kusaidia kukupata. Ila hatudhani kuwa itakuwa hivyo. Tunataka wewe uwe mmoja wa kutusaidia kumpata muuaji wa mpenzi wako, sawa?" Koplo Peter alimaliza.

Donald aliingia kwenye gari lake na kuendesha kwa kasi kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi hadi maeneo ya Namanga kwa Doroth. Alimkuta kwa sababu alimpigia simu kuwa anakwenda kwake.

Kwa mara ya kwanza Doroth alipata furaha isiyo kifani kusikia kuwa Donald anakwenda nyumbani kwake. Alijua kuwa sasa mapenzi yanarudi upya. Alijipongeza kwa mpango wake kabambe yeye na wakwe zake wa kumaliza Tausi.

Donald aliingia sebuleni na kumkuta Doroth akiwa ameketi kwenye kochi akinywa juisi.

"Karibu mpenzi." Alimkaribisha.

Donald alimuangalia kwa jicho kali kidogo, akaenda kukaa pembeni mwa kochi.

"Mbona kama umekasirika, wakati umeniambia leo unakuja nyumbani, una mazungumzo na mimi mpenzi?"

"Mpango wenu nimeubaini"

"Unasemaje?"

"Ndiyo, wewe, baba na mama mmeshirikiana kumuua Tausi."

Ulikuwa ni mshtuko mkuu kwa Doroth. Ni kweli alijua kuna siku ukweli unajulikana, lakini si mapema kiasi hicho. Alijiandaa kwamba kumtia mikononi Donald na baadaye hapo kutumia gharama kubwa kuulinda ukweli. Lakini sasa umejulikana.

"Mimi nimemuua Tausi? Nani kakwambia?"

"Unadhani duniani kuna siri. Kumbe simu yangu haikupotea kwa bahati mbaya. Ilichukuliwa na kufichwa. Mkampigia simu mtoto wa watu kumdanganya kuwa mimi namwita Sinza kwa kutumia simu ya mtu mwingine naye ni baba yangu mzee Peterson, na mkachukua fursa hiyo kumuua. Yote haya kwa sababu ya kuwa hukutana awe na mimi. Wewe ndiye ulitaka uwe na mimi. Doroth siku zote kumbuka mapenzi hayalazimishwi." Donald akasema na kumuacha kwanza yamuingie.

"We mbona mimi sikuelewi?"

"Ndiyo unanielewa leo. Mko karibuni kukamatwa."

"Kwani suala hili polisi wanalijua?"

"Hivi umewafanya polisi hawajui kazi yao? Hawajajua kuwa wewe, baba na mama mmemuua Tausi, lakini muda si mrefu watajua na kuwatia mbaroni."

"Hivi we Donald leo umenifuata nyumbani kwangu ukiwa umekunywa?"

"Sijakunywa, ila nawaambia tabia mlioifanya sijaipenda na si nzuri na hivi tu kwa sababu waliofanya hivyo ni baba na mama, vinginevyo saa hizi ningekuwa nimeshalibwaga jambo hili polisi."

Hofu kidogo ilimuondoka Doroth akijua Donald hatoweza kusema jambo lile polisi kwa sababu asingependa wazazi wake wakamatwe.

"Na hili nenda kawaambie wenzio kuwa nimejua."

"Si uende ukawaambie mwenyewe uongo wako wazazi wako."

"Siwaambii, ila siku wakitiwa pingu na wewe mwenyewe ndiyo mtajua."

**INAENDELEA JUMAPILI**




CHEZA USHINDE KASINO



# SHAMSA FORD OMBA MUNGU WANAUME WASIKUPE MAJARIBU

MWIGIZAJI wa filamu za Bongo Muvi, Shamsa Ford, ameibua mjadala mkali baada ya kuwataja wanaume wa Kitanzania kuwa wana pesa, heshima, wahuni na waongo.

Kupitia kurasa yaake ya WhatsApp, Shamsa, amemweleza rafiki yake aliyemtaja kwa jina la Anita, asiwe na mawazo ya kuja Tanzania na kukumbana na wanaume wa huku kwani atakiona cha moto.

"Una bahati Anita, una mwanaume bilionea, anakupa unachotaka , anakulea kama malkia, anakupenda na kukuheshimu aisee mshikilie, njoo Bongo tukuhadithie wanaume wetu ukiwaomba pesa wananuna"

Ameongeza "yakiwa hayana eti yanasema nakupima, sasa unampima halafu shida zake ziende wapi? Wahuni, waongo, hawana heshima. Wanaume wa kibongo msinitongoze sitaki,"



# Ibraah umeanza kwenye Instagram, halafu...

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, kutoka lebo ya Konde Gang, Ibraah, amefunguka kuhusu uvumi unaosambaa kwamba ana uhusiano wa kimapenzi na Fahyma, ambaye ni mama mtoto wa Rayvanny.

Ibraah amesema kitendo cha kuweka picha ya mrembo huyo katika akaunti yake ya Instagram haimaanishi kwamba tayari wanatoka kimapenzi, bali ni mahaba tu ya kawaida.

"Unajua Fahyma ni mwanamke wa Kitanzania, kila mtu ana haki ya kumuonyesha upendo, lakini sijafikiria kuanzisha nae uhusiano wa kimapenzi," amesema Ibraah.

HABARI MICHEZO

LIVE IN PLAY
BET MECHI IKIENDELEA USHINDE.

SPORTPESA APP
CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA




MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 22 - AGOSTI 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 4076 | Twente vs Ajax | 8.51 | 5.94 | 1.27 |
| 14:00 | 1016 | Dundee FC vs Hibernian | 3.95 | 3.60 | 1.84 |
| 14:00 | 5911 | Lyon vs Clermont Foot | 1.59 | 4.16 | 5.15 |
| 15:00 | 3722 | Randers vs Aalborg | 2.50 | 3.44 | 2.60 |
| 15:30 | 3891 | Feyenoord vs GO Ahead Eagles | 1.25 | 5.93 | 9.69 |
| 16:00 | 1063 | Bordeaux vs Angers | 2.79 | 3.19 | 2.54 |
| 16:00 | 1654 | Wolverhampton vs Tottenham | 3.12 | 3.12 | 2.42 |
| 16:00 | 1689 | Elfsborg vs Hammarby | 2.19 | 3.33 | 2.95 |
| 16:00 | 2128 | Southampton vs Manchester Utd | 4.78 | 4.01 | 1.68 |
| 16:00 | 2193 | Metz vs Reims | 2.31 | 2.94 | 3.43 |
| 16:00 | 3408 | Montpellier vs Lorient | 2.18 | 3.23 | 3.38 |
| 16:00 | 4205 | Lokomotiv Moscow vs FC Krasnodar | 2.42 | 3.21 | 2.86 |
| 16:00 | 5530 | Strasbourg vs Troyes | 2.02 | 3.34 | 3.69 |
| 16:30 | 1206 | Hoffenheim vs Union Berlin | 1.98 | 3.59 | 3.54 |
| 17:00 | 3142 | Hearts vs Aberdeen | 2.14 | 3.11 | 3.50 |
| 17:00 | 3186 | Ross County vs Rangers | 10.82 | 5.70 | 1.24 |
| 17:00 | 4070 | Copenhagen vs Sonderjyske | 1.29 | 5.32 | 8.87 |
| 17:00 | 4765 | St Johnstone vs Dundee Utd | 2.06 | 3.21 | 3.61 |
| 17:30 | 1077 | Servette Geneva vs FC Luzern | 2.18 | 3.68 | 2.90 |
| 17:30 | 1483 | Vojvodina vs Novi Pazar | 1.59 | 3.98 | 4.66 |
| 17:30 | 2621 | Tondela vs Portimonense | 2.78 | 2.87 | 2.73 |
| 17:45 | 5929 | Vitesse Arnhem vs Willem II Tilburg | 1.61 | 3.96 | 4.95 |
| 18:00 | 1313 | Rennes vs Nantes | 1.86 | 3.53 | 4.08 |
| 18:00 | 3910 | Sturm Graz vs Austria Vienna | 1.60 | 4.07 | 4.46 |
| 18:00 | 4112 | Real Sociedad vs Rayo Vallecano | 1.48 | 4.44 | 6.45 |
| 18:00 | 4970 | Nizhny Novgorod vs Rostov | 2.96 | 3.01 | 2.47 |
| 18:00 | 5276 | Rapid Vienna vs Josko Ried | 1.42 | 4.55 | 5.81 |
| 18:30 | 2856 | Arsenal vs Chelsea | 4.62 | 3.67 | 1.77 |
| 18:30 | 3226 | Bayern Munchen vs FC Koln | 1.12 | 8.56 | 16.92 |
| 18:30 | 5198 | AIK Football vs BK Hacken | 1.91 | 3.34 | 3.68 |
| 19:00 | 4873 | Valerenga vs Viking | 1.76 | 3.75 | 4.14 |
| 19:00 | 5323 | Haugesund vs Lillestrom | 2.00 | 3.51 | 3.46 |
| 19:00 | 5579 | Viborg FF vs Aarhus | 2.50 | 3.14 | 2.80 |
| 19:15 | 1561 | Konyaspor vs Basaksehir | 2.57 | 2.97 | 2.87 |
| 19:30 | 1582 | Udinese vs Juventus | 6.06 | 4.16 | 1.54 |
| 19:30 | 4828 | Brugge vs Kfco Wilrijk | 1.17 | 6.90 | 12.82 |
| 19:30 | 5510 | Bologna vs Salernitana | 1.63 | 4.02 | 5.22 |
| 20:00 | 1677 | FK Khimki vs Rubin Kazan | 3.05 | 3.10 | 2.35 |
| 20:00 | 2312 | Maritimo vs Porto | 8.05 | 4.71 | 1.35 |
| 20:30 | 4861 | Atletico Madrid vs Elche | 1.24 | 5.64 | 14.11 |
| 21:00 | 3611 | Rosenborg vs Odd Ballklubb | 1.59 | 4.14 | 4.93 |
| 21:45 | 1998 | Napoli vs Venezia | 1.24 | 6.39 | 10.99 |
| 21:45 | 2063 | Goeztepe vs Yeni Malatyaspor | 2.15 | 3.16 | 3.41 |
| 21:45 | 2235 | Nice vs Marseille | 2.64 | 3.24 | 2.64 |
| 21:45 | 2543 | Fenerbahce vs Antalyaspor | 1.50 | 4.33 | 5.71 |
| 21:45 | 3002 | Roma vs Fiorentina | 1.76 | 3.92 | 4.32 |
| 22:00 | 3336 | Mechelen vs Union Saint Gilloise | 3.49 | 3.49 | 1.99 |
| 22:00 | 4040 | Kolubara vs Partizan | 8.51 | 4.74 | 1.31 |
| 22:30 | 1534 | Vitoria Guimaraes vs FC Vizela | 1.68 | 3.61 | 4.94 |
| 23:00 | 5503 | Levante vs Real Madrid | 4.69 | 4.02 | 1.69 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# COURTOIS MITANO TENA MADRID



**MADRID,** Hispania

GOLIKIPA Thibaut Courtois amekubali kusaini mkataba mpya wa miaka mitano na Real Madrid.

Madrid wameruhusu mabeki wenye uzoefu Sergio Ramos na Raphael Varane kuondoka klabuni, kwani wanatafuta kupunguza tatizo la kifedha lililoongezwa na janga la virusi vya corona.

Lakini, Madrid wameamua kupata mustakabali wa muda mrefu wa Courtois, ambaye amesaini mkataba mpya, huku ule wa awali ulikuwa unamalizika Juni 30, 2026.

Courtois alijiunga na Madrid akitokea Chelsea mwaka 2018, baada ya kufanya vyema na Ubelgiji kwenye Kombe la Dunia huko Urusi ambapo alishinda tuzo ya golikipa bora 'Golden Glove'.

Ameendelea kujitambulisha kama namba moja wa Los Blancos baada ya mwanzo mgumu mwanzoni mwa msimu wa pili huko LaLiga - Courtois akiwa amechezea Atletico Madrid kwa mkopo kutoka Chelsea.

Mchezaji huyo huyo mwenye umri wa miaka 29 amesaidia Madrid kutwaa mataji matatu, kushinda LaLiga mwaka 2019-20, Supercopa de Espana msimu huo na Kombe la Dunia la Klabu ya FIFA ya 2018.



# Solskjaer: Martial atathibitisha uwezo

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amemuunga mkono Anthony Martial kuthibitisha mashaka yake kuwa na makosa na anaamini mashabiki wataona mchezaji tofauti na yule wa msimu uliopita.

Solskjaer alikanusha kuwa mshambuliaji huyo anaweza kuondoka klabuni kabla ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho huu na kuelezea ni kwanini ana matumaini msimu huu utakuwa tofauti kwa Martial.

Solskjaer aliulizwa katika mkutano wake na waandishi wa habari ikiwa anafikiria Martial ana kile kinachohitajika kuwa namba 9 wa Manchester United.

Alijibu: "Kama nilivyosema kabla tunajua uwezo wa Anthony. Msimu uliopita ulikuwa mbaya, tulikuwa na majeraha, alipoteza kiwango, kabla ya kuwa mfungaji bora wetu.

"Kama Anthony atapiga penalti zote, au Marcus Rashford angepiga penalti zote msimu uliopita hayo ni mabao mengine 10-15 kwa mshambuliaji wa kati, lakini tuna Bruno (Fernandes) ambaye anajiamini sana kwenye penalti huwezi kumzuia kwa kweli.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI UWANJANI PARIS WIKI IJAYO

Utakuwa mchezo wake wa kwanza wakati PSG itakapokuwa ugenini dhidi...

**PARIS,** Ufaransa

MASHABIKI wa Paris Saint-Germain na wengine ulimwenguni watalazimika kusubiri wiki zaidi ili kuona Lionel Messi akicheza mechi yake ya kwanza na klabu yake mpya.

Katika mchezo wa juzi Ijumaa, kocha Mauricio Pochettino hakumtaja katika kikosi cha klabu hiyo kilichocheza dhidi ya Brest na kuibuka na ushindi wa mabao 4-2.

Neymar na Leandro Paredes wote walikosa mechi hiyo pia na wawili hao wamefika fainali ya Copa America na hawakuwa na msimu wa mapema.

**Habari kuwa Messi hakuwapo kwenye orodha hiyo kuna maana kwamba atacheza kwenye mechi ya nne ya Ligue 1 ya msimu, ambayo itakuwa dhidi ya Stade de Reims ugenini Agosti 29, mwaka huu.**

Hii itakuwa kabla ya mapumziko ya kwanza ya kimataifa ya kampeni, ambapo Messi anatarajiwa kuiongoza Argentina katika kufuzu Kombe la Dunia la 2022 dhidi ya Venezuela, Brazil na Bolivia.

Messi alibaki jijini Paris, akifanya mazoezi, wakati wachezaji wenzake walisafiri kwenda Brittany kujiandaa na pambano hilo la Ligue 1.

Mbali na Paredes na Neymar, Sergio Rico pia alikosa akifungua mlango kwa Gianluigi Donnarumma kuanza na PSG.

## KWA UFUPI

### VESTERGAARD MAMBO SAFI

KLABU ya Southampton imekubali dau la pauni milioni 15 kutoka kwa Leicester City kumwachia mlinzi wake raia wa Denmark, Jannik Vestergaard mwenye umri wa miaka 29. (Daily Echo)

### SPURS, VILLA VITANI

TOTTENHAM Hotspur na Aston Villa wote wanaandaa ofa kwa kiungo wa Southampton mwenye umri wa miaka 26 raia wa England, James Ward-Prowse (Telegraph)

### SHAQIRI ATAJWA LYON

LYON wanafanya mazungumzo na Liverpool juu ya makubaliano ya kumsajili kiungo wa wekundu hao mwenye umri wa miaka 29, Xherdan Shaqiri. (Sky Sports)

### KEANA ATAKIWA INTER

INTER Milan wana nia ya kumsajili mshambuliaji wa Everton mwenye umri wa miaka 21, raia wa Italia, Moise Kean, ambaye alicheza msimu uliopita kwa mkopo katika klabu ya PSG. (Sky Sports)

### CITY, KANE NGOMA MBICHI

MANCHESTER City imesisitiza bado inamlenga zaidi mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na Timu ya Taifa ya England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28. (Mirror)

### RAMSDALE AJADILIWA

ARSENAL imeanzisha tena mazungumzo na Sheffield United juu ya makubaliano ya mlinda mlango wa England, Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 23. (The Athletic)

### PSG, POGBA HAKULA KULALA

KLABU ya Paris St-Germain haijaondoa uwezekano wa uhamisho wa dakika za mwisho wa viungo wa kati raia wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28 kutoka Manchester United na Eduardo Camavinga wa Rennes. (L'Equipe)

### MBAPPE SOKONI

PSG ina nia ya kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, kwa Real Madrid msimu huu. (Mundo Deportivo)

### ZOUMA ANUKIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inafikiria uhamisho wa mlinzi wa Chelsea, Kurt Zouma. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 26, pia anahusishwa na uhamisho wa West Ham msimu huu. (Sky Sports)

### ATLETICO: TRIPPIER HAUZWI

KLABU ya Atletico Madrid imeziambia Arsenal na Manchester United kwamba, beki wa kulia wa England, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 30, hauzwi. (AS)

### GUEDES ANUKIA EPL

KLABU ya Wolverhampton Wanderers inajitayarisha kutoa ofa ya pauni milioni 21 kwa Valencia ikimlenga winga wa Ureno, Goncalo Guedes, mwenye umri wa miaka 24. (Birmingham Mail)

### BRUCE AMTAKA CHOUDHURY

KOCHA wa Newcastle, Steve Bruce anamwinda kiungo wa kati wa Leicester, Hamza Choudhury mwenye umri wa miaka 23 kwa mkopo. (Mail)

### RODRIGUEZ: SIONDOKI

NYOTA wa Everton, James Rodriguez amekanusha taarifa kuwa anatafuta uhamisho wa kwenda Atletico Madrid, baada ya ujumbe wa Twitter wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 raia wa Colombia kuchukuliwa kama kidokezo kwamba anahamia kwa mabingwa hao wa La Liga. (Liverpool Echo)

# NDAYIRAGIJE AREJEA TENA LIGI KUU TANZANIA BARA

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) Mrundi Etienne Ndayiragije, anatarajiwa kuanza kibarua kipya cha kuifundisha Geita Gold FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara hapo kesho Jumatatu, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Geita Gold FC, George Mbiligeda, alisema Ndayiragije ameshasaini mkataba wa mwaka mmoja na timu hiyo baada ya kufikia makubaliano.

Mbiligeda alisema uamuzi wa kumwajiri kocha huyo ni katika malengo ya kukiimarisha kikosi chao pamoja na usajili mzuri ambao wameufanya kuelekea msimu mpya.

Kiongozi huyo alisema wanafahamu uwezo wa kufundisha wa kocha huyo, ni mwalimu ambaye anaifahamu vizuri Ligi Kuu Tanzania Bara na wachezaji wengine wanaoichezea kutokana na historia yake.

"Etienne kwa sasa ni kocha wetu na ataanza kazi rasmi Jumatatu (kesho), usajili wa wachezaji umekamilika kwa asilimi 90 na kazi kubwa iliyopo kwa wachezaji na kocha ni kuingia kazini kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa ligi," alisema Mbiligeda.

Aliongeza Ndayiragije atashirikiana na makocha wengine walikuwapo kwenye benchi la ufundi ambalo amelikuta kwa ajili ya kufikia malengo ya timu ambayo ni kufanya vizuri.

"Tunajua kutokana na udhamini wa Azam Media kuweka fedha nyingi, ligi itakuwa na ushindani mkubwa, timu zimefanya usajili na kujipanga vizuri, kulitambua hilo tumekuwa makini katika usajili wetu wa wachezaji pamoja na kuboresha benchi letu la ufundi," alisema Mbiligeda.

Geita Gold FC ya mkoani Geita pamoja na Mbeya Kwanza ni timu zilizopanda daraja, hivyo zitashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza kwenye msimu wa 2021/22.

Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao itashirikisha jumla ya timu 16 ambazo ni pamoja na mabingwa Simba, Yanga, Azam FC, Biashara United, KMC, Polisi Tanzania, Kagera Sugar, Mtibwa Sugar, Dodoma Jiji, Ruvu Shooting, Coastal Union, Tanzania Prisons, Namungo FC Mbeya City, Geita Gold na Mbeya Kwanza.



Kiungo mkabaji wa Simba Queens, Fatuma Issa (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Timu ya Vijana ya Ukonga City (U-15), katika mechi ya kirafiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa JKM Park jijini Dar es Salaam jana. Simba Queens ilishinda mabao 3-0. **PICHA: SIMBA SC**

# Simba Queens kuanza na Warundi

**Na Saada Akida**

MABINGWA wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens, wataanza kuwania ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) kwa kuvaana na PVP FC ya Burundi katika mechi itakayochezwa Jumamosi Agosti 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nyayo jijini Nairobi, Kenya.

Michuano hiyo itakayoshirikisha timu tisa za Ukanda wa CECAFA itatoa mwakilishi atakayeshiriki Fainali za Klabu Bingwa Afrika baadaye mwaka huu nchini Misri.

Wawakilishi hao wa Tanzania Bara, Simba Queens watashuka tena dimbani Agosti 31, mwaka huu kucheza dhidi ya Lady Doves WFC na Septemba 3, mwaka huu watamaliza mechi za hatua ya makundi kwa kuvaana na FAD FC ya Djibouti.

Mechi ya ufunguzi ya michuano hiyo itakayomalizika Septemba 9, mwaka huu itakuwa ni kati ya Lady Doves WFC dhidi ya FAD FC, zote kutoka Kundi A.

Timu zilizoko Kundi B ni pamoja na Yei Joint Stars FC, New Generation FC ya Zanzibar, Kikosi cha Benki ya Biashara Ethiopia na wenyeji Vihiga Queens.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Hababuu Ali aliliambia gazeti hili wanatarajiwa kuondoka nchini kuelekea Kenya Jumatano au Alhamisi na wako tayari kwenda kuliwakilisha vizuri taifa.

# Makambo ajipa jukumu Yanga

**Na Adam Fungamwango**

BEKI mpya wa Yanga, Yannick Bangala, amesema anajisikia furaha kukutana na wachezaji wenzake wa zamani wa AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) akiwamo Heritier Makambo ambaye amekuwa mwalimu wake wa Kiswahili wakiwa kambini nchini Morocco.

Akizungumza baada ya kutambulishwa rasmi huko Morocco, Bangala alisema anajiona hapo Yanga ni sawa na nyumbani kwa sababu amekutana na wachezaji aliokuwa nao AS Vita, ambapo yeye alikuwa nahodha wao.

Wachezaji wa AS Vita ambao alikuwa nao Bangala ni pamoja na Djuma Shaaban, Fiston Mayele na Jesus Moloko.

"Yanga ni timu nzuri. Najisikia vizuri kuichezea. Nimefurahi sana kuja kuichezea timu hii. Ni timu kubwa, najivunia kujiunga nayo, naahidi kuisaidia kwenye michuano mbalimbali kwa kushirikiana na wenzangu ili kushinda mataji," alisema mchezaji huyo.

Alisema ushirikiano na wachezaji wenzake katika kikosi hicho ni mkubwa lakini nyota wenzake kutoka DRC wamesaidia yeye kutojiona mgeni.

"Wengine nilikuwa nao AS Vita na mimi nilikuwa nahodha wao, Makambo yeye tulicheza ligi moja tukiwa Congo DR, na yeye amekuwa akinisaidia sana kwenye lugha ya kiswahili," alisema beki huyo.

# Badru, Mtibwa bado wajiuliza

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Mohammed Badru, amesema hatima ya ajira yake ndani ya timu hiyo iko mikononi mwa viongozi wa timu hiyo huku maandalizi ya msimu mpya yakitarajiwa kuanza.

Badru amemaliza mkataba wa muda mfupi aliokuwa ameingia na timu hiyo, na mazungumzo ya kusaini mkataba mpya bado hayajafikia tamati.

Kocha huyo alisema yeye bado anaipa kipaumbele Mtibwa Sugar ambao wameonyesha nia kuendelea kuwaongoza.

Alisema tayari ameshapokea ofa kutoka katika timu tatu (hakuna tayari kuzitaja), lakini moyo wake unapendelea kubakia Mtibwa Sugar kama hakutakuwa na uamuzi mwingine tofauti.

"Endapo Mtibwa Sugar watabadilisha uamuzi basi nitarudi Uingereza kwenda kuendelea na ajira yangu ya kufundisha Woodford Town FC, U-21, inashiriki Ligi ya Vijana ya FA, bado nina mkataba nao, nimekuja huku kutembea lakini kutokana na changamoto za COVID 19 nilishindwa kuondoka,"

Kocha huyo aliisaidia Mtibwa Sugar kujinusuru na janga la kushuka daraja kwa kuzinduka kwenye michezo ya lala salama.

# Michezo

Jumapili Agosti 22, 2021

Nipashe





## Messi uwanjani Paris wiki ijayo

HABARI UK 22

# Kanoute abeba matumaini

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imeonyesha kufurahishwa na usajili wa mchezaji, Sadio Kanoute raia ya Mali na kusema ni moja kati ya nyota watano bora waliowahi kutua klabuni hapo katika miaka ya karibuni.

Kaimu Ofisa Habari wa Simba, Ezekiel Kamwaga, aliliambia gazeti hili wanajivunia kumpata mchezaji huyo bora barani Afrika, ambaye anatarajiwa ataongeza nguvu na imani ya kuendelea kuwa na matokeo mazuri katika msimu ujao kuliko walivyofanya kwenye msimu uliopita.

"Kama nilivyosema kuna watu wana uzoefu mkubwa kwenye kazi ya usajili kwenye klabu yetu. Usajili wa mchezaji huyu ni mkubwa sana. Si tu kwamba anakuja kuichezea Simba peke yake, anakuja kwenye timu ambayo ameshaitazama, akishirikiana na anayewakuta kufika mbali kwenye mafanikio," alisema Kamwaga.

Alisema Simba haisajili tu ili kujaza nafasi, bali inasajili wachezaji kwa kuzingatia matakwa ya benchi la ufundi na maslahi mapana ya klabu.

"Simba inaangalia miaka mitatu au minne mbele. Na msimu ujao malengo yetu ni kuchukua makombe yote ya nchini, halafu kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kwa sababu tumefika mara mbili hatua ya robo fainali, sasa tunaitaka nusu fainali, fainali au ikiwezekana kutwaa kabisa ubingwa, kinyume na hapo, malengo yatakuwa hayajatimia," Kamwaga aliongeza.

Kiongozi huyo alisema bado hawajamaliza kutambulisha wachezaji na muda utakapofika, wataweka wazi wachezaji ambao majina yao yamekwenda Shirikisho la Soka Afrika (CAF), na wale ambao usajili wao utakuwa ni kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara.



Bondia Twaha Kiduku (kushoto) kutoka Morogoro, akimpiga ngumi mpinzani wake, Dulla Mbabe, katika pambano lililofanyika kwenye ukumbi wa Ubungo Plaza jijini Dar es Salaam usiku wa kuamkia jana. Twaha alitangazwa mshindi na kupata zawadi ya gari aina ya Crown. **PICHA: MTANDAO**

# KIVULI CHA MIQUISSONE CHATESA

## Yanga yamkana nyota huyo huku Simba ikisema watani zao hawana...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI utambulisho rasmi haujafanyika kuhusiana na timu mpya atakayotua aliyekuwa winga wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Luis Miquissone haujafanyika, 'kivuli' cha nyota huyo bado hakijafutika kwa mashabiki wa soka hapa nchini.

Tayari Miquissone ameshaaga rasmi mashabiki wa Simba na klabu hiyo ikimtakia kila la kheri katika timu yake mpya atakayojiunga.

Vyombo vya habari juzi jioni viliripoti Miquissone pamoja na nyota mwingine raia wa Afrika Kusini, Percy Tau, wanatarajiwa kutua Cairo, Misri mapema wiki ijayo baada ya kukamilisha uhamisho wa kujiunga na mabingwa wa Afrika, Al Ahly.

Hata hivyo kutokana na historia na Simba na Yanga kunyang'anyana wachezaji, mashabiki wa Wekundu wa Msimbazi wamekuwa na hofu nyota huyo huenda akatambulishwa katika siku ya kilele cha Wiki ya Mwananchi itakayofanyika Agosti 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema klabu yake imeshamaliza mchakato wa usajili katika msimu wa 2021/22, na Miquissone si sehemu ya kikosi chao chenye wachezaji 28.

Bumbuli alisema Yanga hawajawahi kutamka au kumtangaza mchezaji mwingine yoyote kwenye kilele cha Wiki ya Mwananchi ambaye hakutambulishwa mapema.

Kiongozi huyo alisema wao wamejiandaa kuonyesha 'sapraizi kubwa', lakini hawajawahi kusema tukio hilo litahusisha kumtangaza mchezaji yoyote yule kinyume na wale ambao wameshawasajili.

**"Tumesema tumekamilisha idadi ya wachezaji 28 kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu. Hayo mengine yanayoanzishwa kwenye mitandao ya kijamii sisi hatuyajui. Haiwezekani yazushwe huko, halafu sisi ndiyo tutoe ufafanuzi. Huko huko yanakozushwa ndiyo ingefaa waulizwe. Sisi tumebakisha nafasi mbili ambazo tutazijaza wakati wa dirisha dogo la usajili kwa sasa tayari tumefunga." alisema Bumbuli.**

Aliongeza anawaomba wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kujitokeza katika kilele cha Wiki ya Mwananchi na kuwataka wajiandae kuona mambo mazuri yatakayoweka historia mpya kwenye soka hapa nchini.

"Nawasisitiza mashabiki wa Yanga kutoka sehemu mbalimbali nchini na hata nje ya Tanzania, Wiki ya Mwanachi si ya kukosa, itakuwa balaa," Bumbuli aliongeza.

Miquissone ambaye msimu uliopita aliisaidia Simba kufanya vyema katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, alitua nchini kwa mkopo akitokea Mamelodi ya Afrika Kusini.

Simba na Yanga zimekuwa na tabia ya kuibiana wachezaji, hasa pale nyota husika anapoonekana kuwa na mchango mkubwa katika timu yake.

Msimu uliomalizika, Yanga ilijaribu kumsajili aliyekuwa kiungo wa Simba, Clatous Chama, raia wa Zambia, lakini mchakato wa uhamisho ulishindikana kwa sababu ya mkataba ambao alikuwa ameshaingia na klabu hiyo.

Hata hivyo, kuonyesha Yanga ilihitaji nyota huyo, picha ya Chama akiwa na jezi ya kijani iliwekwa katika ukurasa wa kwanza wa jarida linalomilikiwa na klabu hiyo.

Wakati huo huo, Ofisa Mhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz, amesema uamuzi wa kuanza sherehe za Wiki ya Wananchi Visiwani Zanzibar ni kuendelea kudumisha amani, upendo na mshikamano wa Tanzania Bara na Wazanzibari.

"Yanga ni moja, Tanzania ni moja, Yenye mshikamo, Zanzibar tunakuja kufanya kile kilichobora, kilele cha Wiki ya Wananchi 2021, sisi tuna watu," Nugaz alisema.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042